ISSN 0856-0323

MWAKA WA 71,
TOLEO NA. 14

GAZETI

6 Aprili, 1990

BEI SH. 10/-

LA

DAR ES SALAAM

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Linatolewa kwa Idhini ya Serikali na
Kuandikishwa Posta kama
Gazeti

YALIYOMO

	Taarifa ya Kawaida	Uk.
Kuajiriwa na Kukabidhiwa Madaraka	Na. 184	87
Notice *re* Supplement	Na. 185	88
Tanzia		88
Court of Appeal of Tanzania at Mbeya Amended—Cause List	Na. 186	88
Matokeo ya Uchaguzi Mdogo Lindi Mjini	Na. 187	89
Kupotea kwa Hati za Kumiliki Ardhi	Na. 188	89
Ubatilisho wa Hati ya Kumiliki Ardhi	Na. 189-90	89
Uvumbuzi Usiigwe	Na. 191-2	89
Mitihani ya Serikali inayoendeshwa na Tume Kusimamishwa	Na. 193	90
Uchunguzi wa Migogoro ya Kikazi ..	Na. 194-7	90/99
Uthibitisho na Usimamizi wa Mirathi	Na. 198-206	100/2
Deed Poll (Change of Name)	Na. 207	102
Mali Isiyo na Mwenyewe	Na. 208	102

KUAJIRIWA NA KUKABIDHIWA MADARAKA

TAARIFA YA KWAIDA NA. 184

Ofisi ya Rais—(Utumishi):

Kuwa Makarani wa Masjala:—

PASKALIS GABONE, kuanzia tarehe 1 Oktoba, 1988.
SHEBA E. MAGULU, kuanzia tarehe 14 Novemba, 1988.
DOMINICK KIMANZI, kuanzia tarehe 28 Oktoba, 1988.
SEVERINA SHIRIMA, kuanzia tarehe 3 Januari, 1989.
ANNA J. L. KISAMBA, kuanzia tarehe 21 Aprili, 1989.

Kuwa Mhasibu Msaidizi:—

JANATH ALLY, kuanzia tarehe 2 Agosti, 1988.

Kuwa Karani wa Hesabu:—

MARTIN MAIGE, kuanzia tarehe 9 Juni 1989.

Kuwa Mpiga Taipu II:—

ANNETH A. MAMUYA, kuanzia tarehe 15 Juni, 1988.

Kuwa Wapiga Taipu III:—

JANE MASWE, kuanzia tarehe 15 Juni, 1987.
GODLIVER KYARUZI, kuanzia tarehe 15 Juni, 1987.
KETINA MWAITEKELE, kuanzia tarehe 15 Juni, 1987.
THEOPIST MWINGIRA, kuanzia tarehe 15 Juni, 1988.
C. MAYALLA, kuanzia tarehe 15 Juni, 1988.
SHITA MADALALI, kuanzia tarehe 15 Juni, 1988.
SALIMA HUSSEIN, kuanzia tarehe 15 Juni, 1988.

Kuwa Librarian:—

PAPIANUS P. M. DEUSDEDIT, kuanzia tarehe 15 Juni, 1988.

Kuwa Tech. Aux.:—

JOYCE MWAIMU, kuanzia tarehe 22 Agosti, 1988.

Kuwa Mwandishi Mahsusi Daraja la III:—

CATHERINE KALINDAGA, kuanzia tarehe 1 Mei, 1989.

Kuajiriwa na Kukabidhiwa Madaraka—(inaendelea tazama ukurasa wa 102)

Matangazo yahusuyo mali za watu waliofariki, kuvunja mikataba ya ushirikiano na mengineyo, yakiwa ya manufaa kwa umma yaweza kuchapishwa katika *Gazeti*. Yapelekwe kwa **Mhariri, Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Utumishi, S.L.P. 2483, Dar es Salaam, Simu za Ofisi 20781/4.** *Kabla ya Jumamosi ya kila Juma.*

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 185

Notice is hereby given that By-laws, an Order and a Notice as Set out below, have been issued and are published in Subsidiary Legislation Supplement No. 13 dated 6th April, 1990 to this number of the Gazette:—

The Lushoto District Council (Development Levy) By-laws, 1989 (Government Notice No. 75 of 1990)

Order under the Public Corporations Act, 1969 (Government Notice No. 76 of 1990)

Notice under the Regulations of Prices Act, 1973 (Government Notice No. 77 of 1990)

TANZIA

Mtukufu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha Ndugu James N. Mwalyambi, Senior Technician kilichotokea huko Morogoro tarehe 22/6/1989.

Mtukufu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha Ndugu Winchslaus B. Clemence, Assistant Technician, kilichotokea Kijijini Kataale huko Bukoba tarehe 7/12/1989.

Mtukufu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo kilichotokea tarehe 16/11/89 cha Ndugu Charles T. M. Ngonyani Mfamasia Dar es Salaam.

Mtukufu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo kilichotokea tarehe 2/1/90 cha Ndugu John M. K. Wakulimpimbwe Daktari Mkoa wa Kagera.

Mtukufu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo kilichotokea 1/2/90, Jijini Dar es Salaam cha Ndugu Chausiku T. Simba Mhudumu wa Ofisi.

Mtukufu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo kilichotokea tarehe 5/3/90 Kibaha cha Ndugu Allan Gilbert Makange Daktari Msaidizi Mwandamizi.

Mtukufu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo kilichotokea tarehe 16/2/90 Kwekivu, wilayani Handeni cha Ndugu Athumani Hamza Mhando — Katibu Tarafa, Wilayani Handeni.

Mtukufu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo kilichotokea tarehe 12/2/90 ghafla kwa ugonjwa huko nyumbani kwake Mbagala, Dar es Salaam cha Ndugu Rogassian R. Killindo, Mkaguzi wa Polisi, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mtukufu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo kilichotokea tarehe 14/2/1990 katika hospitali ya Muhimbili kwa maradhi cha Ndugu R.S.M. Aidan Selemani, askari wa Wizara ya Mambo ya Ndani.

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 186

IN THE COURT OF APPEAL OF TANZANIA
AT MBEYA

AMENDED CAUSE LIST

Before: KISANGA, J. A., RAMADHANI, J. A. AND MNZAVAS, J. A.

Monday the 17th Day of May, 1990
In Court at 9.00 a.m.

For Hearing	*Criminal Appeals*
No. 85/88	C. Siwakwe versus The Republic.
No. 137/89	Godfrey Mwakisu versus The Republic.

Tuesday the 8th Day of May, 1990.

No. 150/87	Ismail Chang Ching versus The Republic.
No. 134/89	The D.P.P. versus Abswedi Bakari

Wednesday the 9th Day of May, 1990.

No. 43/89	Jackson Mwakatoka and others versus The Republic.
No. 150/89	Osaka Joseph Mbedule versus The Republic.

Thursday the 10th day of May, 1990.

No. 129/89	Zabron Nziku versus The Republic
No. 44/89	Charles Sanga versus The Republic.

Friday the 11th day of May, 1990.

No. 151/89	SGT. Masanja Philipho Kija versus The Republic
No. 148/89	Jumapili Yalemela versus The Republic.

Monday the 14th day of May, 1990.

No. 66/88	Jumanne Yusufu Shauritanga versus The Republic
No. 32/88	The D.P.P. versus Jeremia Kalawila Mkiwa

Tuesday the 15th day of May, 1990

Before: MNZAVAS, J. A.
In Chambers at 8.45 a.m.

For Hearing	*Criminal Appeals*
No. MYA 1/89	Jella Kalinga versus Omari Kalumwana

Before: KISANGA, J. A., RAMADHANI, J. A. AND MNZAVAS, J. A.
In Court at 9.00 a.m.

For Hearing	*Criminal Appeals*
No. 149/89	Juma Lwimiko versus The Republic

Dar es Salaam,
21st Machi, 1990

J. H. MSOFFE,
Senior Deputy Registrar

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 187

MATOKEO YA UCHAGUZI MDOGO LINDI MJINI

(Sheria ya Uchaguzi, 1985)

Kwa mujibu wa Fungu la 8 (c) la Sheria ya Uchaguzi Na. 1 ya mwaka 1985, Tume ya Uchaguzi inatangaza kwa taarifa ya watu wote kwamba matokeo ya Uchaguzi Mdogo wa Bunge kwa Jimbo la Uchaguzi la Lindi Mjini, uliofanyika tarehe 25 Machi, 1990 ni kama ifuatavyo:—

	Kura
Ndugu Nakuwa, Saidi Abdallah	1,533
Ndugu Manyanya, Mohamed Nasibu	1,108

Mgombea aliyechaguliwa ni Ndugu Nakuwa Saidi Abdallah.

Dar es Salaam,
27 Machi, 1990

CHIFU A. S. MKWAWA,
Mwenyekiti
Tume ya Uchaguzi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 188

KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI

Sheria ya Uandikishaji wa Ardhi

(Sura 334)

Hati Nambari: 186171/47.

Mmiliki aliyeandikishwa: INDUSTRIAL MANAGEMENT SERVICES LIMITED.

Ardhi: Kiwanja Nambari 598A Upanga Dar es Salaam mjini.

TAARIFA IMETOLEWA kwamba Hati ya Kumiliki iliyotajwa juu imepotea na ninakusudia kutoa Hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa miezi miwili tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika Gazeti la Serikali.

HATI ya asili ikionekana irudishwe kwa Msajili wa Hati Idara ya Hati za Ardhi, S.L.P. 1191, Dar es Salaam.

14 Machi, 1990

S. SINDA,
Asst. Registrar of Titles

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 189

UBATISHO WA HATI YA KUMILIKI ARDHI

Hati ya haki ya kumiliki ardhi juu ya kiwanja Na. 447 Kitalu '46' Kijitonyama Jijini Dar es Salaam ambacho kilimilikiwa na ndugu Samwel Gamaliel imebatilishwa na Waziri wa Ardhi, Maliasili na Utalii kwa niaba ya Mtukufu Rais mnamo tarehe 22 Oktoba, 1989.

Dar es Salaam,
22 Desemba, 1989

MICHAEL MDOE JUMA LUGURU,
Kamishna wa Ardhi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 190

UBATILISHO WA HATI YA KUMILIKI ARDHI

Hati ya kumiliki ardhi yenye L.O. No. 569, CT. No. 5249, Na. 11932 juu ya eneo lenye ukubwa wa karibu ekari 1157 Gonja Wilaya ya Same ambalo lilikuwa linamilikiwa na Messrs Gonja Estates Limited ilibatilishwa kwa amri ya Waziri wa Ardhi, Maliasili na Utalii kwa niaba ya Mtukufu Rais mnamo tarehe 6 Desemba, 1989.

MICHAEL MDOE JUMA LUGURU,
Kamishna wa Ardhi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 191

HATI YA UVUMBUZI

Sheria ya Uandikishaji uvumbuzi usiigwe

(Sura 217)

Inatangazwa kwa watu wote kwamba Hati za Uvumbuzi zenye maelezo yaliyomo kwenye nyongeza ya Tangazo hili ziliandikwa kuwa nambari 2397 ya 1990 katika Daftari la Tanganyika la kuandikisha Hati za Uvumbuzi mnamo tarehe 20 mwezi wa Machi, 1990.

NYONGEZA

Nambari ya Ombi: 2397

Tarehe ya Ombi: 20/3/90

Jina la Mwombaji: SHELL INTERNATIONAL RESEARCH MAATSCHAPPIJ B. V.

Anuani iliyoandikishwa: Carel Van Bylandtlaan 30,2596 HR The Hague, Netherlands.

Maelezo ya kukubaliwa katika Ulaya ya Uingereza: Hati ya Maainisho ya uvumbuzi No. 0171853 ya tarehe 19/2/86 iliyoandikishwa Ulaya ya Uingereza.

Aina ya kitu kilichovumbuliwa: PESTICIDAL BENZOYIUREA COMPOUNDS.

Hati n.k. zilizowasilishwa kwenye Masjala: Hati ya maainisho ya uvumbuzi iliyoandikishwa Ulaya ya Uingereza Hati ya Msimamizi Mkuu wa uvumbuzi Ulaya ya Uingereza. Hati ya Mwakilishi c/o Abdulmalik & Surendra Trade mark & Patent Agents P.O. Box 1132 Dar es Salaam.

Dar es Salaam,

S. D. MTETEWAUNGA,
Msajili Msaidizi wa Uvumbuzi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 192

HATI YA UVUMBUZI

Sheria ya Uandikishaji uvumbuzi usiigwe

(Sura 217)

Inatangazwa kwa watu wote kwamba Hati za Uvumbuzi zenye maelezo yaliyomo kwenye nyongeza ya Tangazo hili ziliandikwa kuwa nambari 2388 ya 1989 katika Daftari la Tanganyika la kuandikisha Hati za Uvumbuzi mnamo tarehe 25 mwezi wa August, 1989.

NYONGEZA

Nambari ya Ombi: 2388

Tarehe ya Ombi: 25/8/89

Jina la Mwombaji: SANDOZ LIMITED.

Anuani iliyoandikishwa: 35 Lichtstrasse CH–4002 Basle Switzerland.

Maelezo ya kukubaliwa katika Ulaya ya Uingereza: Hati ya Maainisho Na. 2138678 ya Uvumbuzi iliyoandikishwa Ulaya ya Uingereza tarehe 19/4/84.

Aina ya kitu kilichovumbuliwa: Pharmaceutical preparation comprising codergocrine and calcium antagonist.

Hati n.k. zilizowasilishwa kwenye Masjala:
1. Hati ya maainisho ya uvumbuzi iliyoandikishwa Ulaya ya Uingereza.
2. Hati ya Msimamizi Mkuu wa uvumbuzi Ulaya ya Uingereza.
3. Hati ya Mwakilishi c/o Donaldson & Wood, Advocates P.O. Box 176 Dar es Salaam.

Dar es Salaam,

E. E. MAHINGILA,
Msajili Msaidizi wa Uvumbuzi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 193

MITIHANI YA SERIKALI INAYOENDESHWA NA TUME KUSIMAMISHWA

Tume ya Utumishi Serikalini iliamua katika kikao Na. 1990/6 kilichofanyika 9/3/1990 kusimamisha mitihani yote inayoendesha hadi hapo itakapotangazwa.

Tume ya Utumishi,
Serikalini,
S.L.P. 9143,
Dar es Salaam, O. SALIM,
23 Machi, 1990. *K.n.y. Mwenyekiti*

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 194

KUH: UCHUNGUZI WA MGOGORO WA KIKAZI NA. 20/1987/88

baina ya

JUMUIYA YA WAFANYAKAZI TANZANIA (JUWATA)

(k.n.y. Wanachama wao 105)

na

TANZANIA TOBACCO "P M B" MOROGORO

(Mwajiri)

UAMUZI

Uchunguzi wa mgogoro huu unawahusu wafanyakazi 106 waliokuwa wanafanya kazi katika kiwanda cha kusindika Tumbaku, Morogoro, wakiongozwa na mmoja wao kwa jina la Cosmas R. Haule. Mgogoro huu ulichunguzwa chini ya kifungu Na. 9A(1) cha sheria ya Mahakama ya Kazi Na. 41/1967 kama ilivyorekebishwa na sheria Na. 18/1977 ili baada ya uchunguzi niletewe taarifa ili nitoe uamuzi chini ya kifungu Na. 9B cha sheria hiyo. Uchunguzi umefanyika kama nilivyoamuru na huu ndiyo uamuzi wangu.

Mlalamikaji Ndugu Haule na wenzake 105 walikuwa wafanyakazi wa Kampuni ya Kusindika Tumbaku iliyoko Morogoro. Waliajiriwa nyakati mbali mbali katika nafasi mbalimbali. Yeye Haule aliajiriwa tarehe 1/4/1968 akiwa 'Record Cleark' kwa mshahara wa Sh. 300/-. Yeye Haule na wenzake walipunguzwa kazi hapo tarehe 1/8/1985. Hawakuridhika na hatua hiyo ya kupunguzwa kazi eti kwa kubana matumizi na kuongeza tija. Walilalamika kuwa kitendo cha menejimenti kilikuwa kinyume na mkataba wa hiari kati ya menejimenti na JUWATA, hivyo kupunguzwa kazi kwao kulikuwa batili. Walalamikaji waliweza kumaliza ngazi zote za malalamiko hayo na hatimaye Kamishna wa Kazi alileta taarifa kwangu na nikaagiza huu uchunguzi ufanyike na katika uchunguzi nilielekeza yafuatayo yatiliwe maanani ili kufikia ufumbuzi wa swala lenyewe:—

(a) Kama Ndugu Haule na wenzake waliachishwa au walipunguzwa kazi.

(b) Kama taratibu za kisheria zilizingatiwa na mwajiri katika kuwaachisha au kuwapunguza kazi Ndugu Haule na wenzake; na

(c) Maswala mengine yoyote ya kisheria yanayojitokeza katika mgogoro huu.

Ili kuweza kudhihirisha madai yao na kukidhi matakwa ya (a) (b) na (c) hapo juu, walalamikaji walitegemea ushahidi wa mtu mmoja, D.W.$_1$ Ndugu Haule ambaye ni kiongozi wa walalamikaji na menejimenti waliita mashahidi wawili (2) DW.$_1$ Mabonyi DW.$_2$ Rajabu S. Mkumba Meneja Utumishi wa bodi ya Tumbaku.

Katika ushahidi wake, PW.$_1$ Haule alisema yeye na wenzake waliachishwa kazi lakini barua ya kuachishwa kazi ya tarehe 13/7/1985 inasema "Yah: KUPUNGUZWA KAZINI" na hati ya kazi ya tarehe 4/7/1985 inasema kuwa sababu ya kuachishwa kazi ni kupunguzwa kazini (redunduncy) vyote vikiwa ni kielelezo P.$_2$ kwa pamoja. Ushahidi huo unajibu swali la kwanza kuwa Ndugu Haule na wenzake walipunguzwa kazi na sio kuachishwa.

Licha ya utekelezaji wa kuwapunguza kazi, walalamikaji wamedai kuwa zoezi hilo ni batili kutokana na mkataba wa hiari kati ya Menejimenti na JUWATA uliotolewa kama kielelezo P.$_3$ na hasa kifungu Na. 7 cha mkataba huo kinachosema:

"KUPUNGUZA WAFANYAKAZI:"

"Pande zote mbili zimekubaliana kwamba juhudi ya pamoja itafanywa ili kulisaidia Taifa katika kupambana na tatizo la ukosefu wa mishahara nchini. Hatua ya kupunguzwa idadi ya wafanyakazi zitachukuliwa tu, iwapo mwajiri ataitosheleza jumuiya kuwa hakuna uwezekeno wowote mwingine wa kuepuka hatua hiyo. Zifuatazo zitakuwa ni hatua miongoni mwa njia zifaazo kufikiriwa juu ya upunguzwaji au uepukaji wa kuwapunguza wafanyakazi, kuwatoa katika sehemu wasizohitajika na kuwaweka katika sehemu ambamo zitaonekana kuwa zina nafasi, au haja ya watu hao, kutoajiri tena kwa muda watu wapya kwa kazi zile zile mpaka hapo hali itakaporudia tena kuwa njema, upunguzwaji wa pole pole kwa wafanyakazi, uchaguzi wa wafanyakazi watakaohusika na upunguzwaji utafuata misingi ya FILO na—

(i) muda wa utumishi

(ii) wafanyakazi ambao wanaachishwa kazi kwa ajili ya upunguzwaji lazima wapewe nafasi ya kwanza kurudishwa kazini wakati mwajiri anapoajiri wafanyakazi wapya."

Kutokana na mkataba huo walalamikaji walidai kuwa menejimenti imekosea kwani (a) walipunguzwa wafanyakazi wa muda mrefu na kuacha walio na muda mfupi kazini. (b) menejimenti waliajiri wafanyakazi wengine na kuwaacha wao waliopunguzwa.

Kabla sijaendelea na muhtasari wa walalamikaji, ningependa kufafanua kuwa hii "FILO" ni neno la kiingereza ambalo kirefu chake ni 'First In Last Out': Hii ina maana kuwa wale wafanyakazi walioajiriwa kwanza watakuwa wa mwisho kupunguzwa. Mkataba huu haukueleza kwa kirefu zaidi kuwa juhudi za wafanyakazi nazo zitatiliwa maanani, kwani unaweza ukapunguza wafanyakazi wenye bidii ya kazi, wanofikia malengo ya kazi na ukaacha wale wasiofikia malengo ya kazi na kusababisha hasara. Hii itakuwa kinyume na nia ya kupunguza ajira na kuongeza tija. Pia kifungu 7(i) cha mkataba kinaeleza kuwa 'muda wa utumishi' bila kuelezea jinsi utakavyotiliwa maanani. Nasema hivyo kwa sababu wakati mwingine watumsihi ambao wamekaribia muda wa kustaafu hupunguzwa kabla ya wale walio na muda mrefu wa kufanya kazi, mradi tu uwezo wao wa kazi ni mkubwa.

Walalamikaji waliendelea kutoa orodha ya wafanyakazi wanaodaiwa kuwa waliajiriwa baada ya walalamikaji kupunguzwa. Hii kama ni kweli ni kinyume cha mkataba wa hiari kielelezo P.$_3$. Orodha ya majina ya wale waliodaiwa kuwa wameajiriwa kwa upya ilitolewa mahakamani na kupokelewa kama kielelezo P.$_4$. Orodha yenyewe ni kama ifuatavyo.

A: *Shipping Department:*

(1) Mohamed Rajabu — Karani (recording Cleark)
(2) Ismail Rajabu — Karani (recording Cleark)
(3) Agnes Kunambi — Karani (recording Cleark)
(4) Hadija Ramadhani — Karani (recording Cleark
(5) Mary Mbaga — Karani (recording Cleark)
(6) Saidi Sabihi — Fork lift driver kutoka TAT Dar es Salaam
(7) Denis Mlema — Fork lift driver kutoka TAT Dar es Salaam

B: *Green Leaf*

(1) Jumanne Selemani — Msimamizi (Supervisor)
(2) Yohana Kakuyu — Msimamizi (Supervisor)
(3) Modest Thomas — Msimamizi (Supervisor)

C: *Leaf Accountants:*

(1) Sala Mapunda — Karani (recording Cleark)
(2) Mariamu Simba — Karani (recording Cleark)
(3) Kashinde Juma — Karani (recording Cleark)
(4) Mhina Ally — Karani (recording Cleark)

D: *Uhasibu (Accounts):*

(1) Abdallah Mwisongo — Karani (Accounts Cleark)
(2) Alcis — Karani (Accounts Cleark)
(3) Abasi Kifeya — Karani (Mishahara)
(4) Adidi D. Lugemalila — Karani Mishahara
(5) Prackseda John — Karani Mishahara
(6) Hussein — (Final Accounts)

E: *Canteen:*

(1) Claudi Kibonge — Mpishi
(2) Maimuna Mohamedi — Mpishi
(3) Susana Daudi — Mpishi
(4) Anna Michael — Mpishi
(5) Anna Augustino — Mpishi
(6) Hilda Chuma — Mpishi
(7) Valelia — Mpishi
(8) Zainabu Nasoro — Mpishi
(9) Zainabu Kidwangi — Mpishi
(10) Sifa Juma — Mpishi
(11) Silivia Chogo — Mpishi
(12) Pili Rashidi — Mpishi
(13) Zainabu Hatibu — Mpishi
(14) Fatuma Mbalika — Mpishi
(15) Amina Marijani — Mpishi

F: *Engineering:*

(1) Ramadhani — M.N. Mechanical (Kudumu)
(2) Mwakatila — Operator
(3) Valery Cosmas — Operator
(4) Mustafa Kassim — Operator
(5) Ngonyani — Operator
(6) Jafary Abdallah — Fundi Umeme
(7) Mase — Fundi Umeme
(8) Godwin Mjema — Fundi bomba
(9) Dalika — Useremala Gr. I
(10) Salum — Operator mashine ya useremala

G: *C & C:*

(1) Shabani Selemani — Operator

H: *Compound:*

(1) Kayombo — Usafi
(2) Stephen Oinary — Driver tractor
(3) Hamisi Ngosha — Usafi

I. *Dispensary:*

(1) Jumanne — Attendant

Katika orodha yote hiyo yenye jumla ya wafanyakazi hamsini (50), ni wafanyakazi watatu (3) tu ambao ni wa kudumu, wakiwa ni Saidi Sabili na Denis Mlema ambao imeelezewa kuwa ni 'Fork lift drivers' waliohamishwa kutoka TAT Dar es Salaam na kupelekwa Morogoro, pamoja na 'fork lift' zao. Hivyo hao hawakuajiriwa kwa upya. Mwingine ni Ramadhani Chamuganda fundi magari ambaye imekubalika kuwa aliajiriwa kwa upya na kuwa kazi yake ni ya kitaalamu ambayo kwamba wote waliopunguzwa hakuna aliyekuwa fundi wa magari. Hata kama wasingelipunguzwa angeliajiriwa. Wengine wote 47 ni vibarua.

Ushahidi mwingine wa walalamikaji ni kuwa menejimenti ilipunguza wafanyakazi wengine iliyokuwa imewapeleka masomoni hasa Ndugu Veneranda Kilua aliyepelekwa uhazili Tabora lakini kutokana na zoezi hili, hakumaliza masomo yake hayo. Wengine ni wale ambao waligharamiwa na mwajiri lakini baadaye walipunguzwa.

Hawani ni:—

(1) Briton Asheri aliyepata mafunzo N.I.P. Mwaka 1979.
(2) Salvatory Masieba—alisoma IDM Mzumbe kwa miaka 2.
(3) Donatian Mutakyarwa na
(4) Theopista Rumisha—Catering Officer kwa muda wa mwaka mmoja.

Ndugu Haule alieleza Mahakama kuwa Mamlaka ya Tumbaku ilivunjwa Aprili, 1985 lakini wafanyakazi wake ambao walitakiwa waachishwe kazi hawakuachishwa bali walihamishiwa katika nafasi zao, baada ya wao kustaafishwa.

Walalamikaji walidai kuwa hawakuweza kuonana na vionbgozi wao wa tawi la JUWATA kutokana na ulinzi mkali. Hatahivyo shauri lao lilifikishwa JUWATA wilayani na kikao cha pamoja kilifanyika 28/8/85 na kikao hicho hakikuleta mafanikio kwa wafanyakazi. Swala hili lilipelekwa kwa Katibu wa JUWATA Mkoa na hadi JUWATA Makao Makuu ambako mgogoro ulitangazwa.

Wakati PW.$_1$ alipohojiwa Mahakamani alikiri kuwa utafiti wake alioufanya mara baada ya zoezi hili ulionyesha kuwa tawi la JUWATA lilishirikishwa na menejimenti kabla ya zoezi lenyewe. Katibu wa tawi aliwakilisha tawi. Shahidi alidai kuwa ingawaje yeye hakuwa mjumbe wa tawi la JUWATA, Hamisi H. Salum alikuwa mjumbe wa tawi na alipunguzwa kazi. Hata hivyo ushahidi ulitolewa na menejimenti kuwa kulikuwa na kibali cha kumpunguza kazi Hamisi Salum kutoka kwa Afisa wa Kazi alichotoa chini ya kifungu Na. 8(b) cha Sheria ya Usalama Kazini, Cap. 574, 1964. Mwisho shahidi alilalamika kuwa kupunguzwa kwao kulikuwa kwa uonevu na hivyo wanaomba warudishwe kazini bila kupoteza haki zao. Huo ulikuwa mwisho wa ushahidi wa walalamikaji.

Menejimenti ambao wanadai kuwa taratibu zote za kuwapunguza kazi wafanyakazi 105 zilifuatwa, waliita mashahidi wawili, DW.$_1$ Maro Mabonyi Katibu wa tawi la JUWATA kiwandani na DW.$_2$ Mkumba, Meneja Utumishi wa Bodi ya Tumbaku Morogoro. DW.$_1$ alieleza Mahakama kuwa yeye alikuwa Kaimu Katibu wa tawi 1984 na mjumbe wa tawi. Walijulishwa na menejimenti kuwa kuna agizo la Serikali la kupunguza ajira ili kubana matumizi na kuongeza ufanisi. Tarehe 3/1/85 walifanya kikao cha pamoja ambacho kiliongelea kwa undani jinsi ya kubana matumizi bila kuathiri ajira ya wafanyakazi. Hata hivyo mwisho walikubaliana kuwa kupunguza ajira ni njia mojawapo ya kubana matumizi. JUWATA ilishiriki kuanzia ngazi ya tawi hadi Bodi ya Wakurugenzi. Pia JUWATA ilikaa na menejimenti katika ngazi ya pili ya utekelezaji, yaani kuchagua wale waliotakiwa kupunguzwa. Na baada ya zoezi hapakuwa na malalamiko

yoyote tawini na tawi halikuwakatalia wafanyakazi wasiwe na vikao nalo. Mwisho $DW._1$ alisema kuwa ni kweli Hamisi Salimu alikuwa mjumbe wa tawi na alipunguzwa kazi baada ya kibali cha afisa wa kazi kama kielelezo $D._{13}$ kinavyoonyesha.

Akihojiwa maswali, $DW._1$ aliendelea kusema kuwa katika vikao vya Bodi mwenyekiti wa tawi ndiye aliyekuwa anahudhuria na kuwa Bodi mbili ya TAT yaani (Tobacco Authority of Tanzania) na T.T.P.C yaani Tanzania Tobacco Processing Company ndizo zilizokuwa zinakaa pamoja, na kulikuwa na jumla ya wafanyakazi 1136 ambako kamati ilitaka 770 wapunguzwe na kubakia 366 tu. Hivyo wengi wao walitakiwa wapunguzwe. Shahidi alisisitiza kuwa katika utekelezaji wa zoezi, walikuwa wanachambua majalada ya wafanyakazi moja moja wakiangalia umri, ujuzi na uzoefu wa kazi. Alisisitiza tena kuwa inawezekana kuwa mfanyakazi mwinginc alikuwa na muda mrefu kazini, lakini alikuwa hana ujuzi. Asingeweza kuachwa kwani hangeweza kuongeza ufanisi, kinyume na agizo la Serikali. Kwa kitendo hicho cha tawi la JUWATA, walikuwa na nia safi ya kukuza uzalishaji mahali pa kazi hivyo kutekeleza wajibu wa mfanyakazi mahali pa kazi.

Kuhusu watu wapya walioajiriwa, shahidi amesema kuwa hakuna kwani yeye yuko kwenye kamati ya ajira na nidhamu. $DW._1$ alifafanua zaidi aina nne za ajira kiwandani hapo kama ifuatavyo:—

(a) Ajira ya wafanyakazi wa kudumu.

(b) Ajira ya msimu—huyu mfanyakazi anaajiriwa tumbaku inapoingia kiwandani. Tumbaku ikiisha na ajira yake inakwisha.

(c) Ajira ya Mkataba ya mwezi—baada ya kufunga msimu, ni zile kazi tu zilizoko kama kusomba magunia na kuyapeleka kwenye ghala. Kazi hiyo ikiisha, basi ajira imekwisha.

(d) Ajira ya Kibarua.

Akiendelea kujibu maswali, shahidi alieleza mahakama kuwa wafanyakazi wote walioko katika orodha kielelezo $P._4$ walikuwa katika ajira ya msimu wa mkataba wa mwezi na sio katika ajira ya kudumu. Hata hivyo, Ramadhani Chamnganda yeye yuko kwenye ajira ya kudumu, kwani yeye ni "Mhandisi" aliyesomea kazi hiyo na Saidi Subihi na Denis Mlama wakiwa "fork lift drivers" walihamishiwa hapo kutoka TAT Dar es Salaam. Jinsi wafanyakazi hao wanavyoajiriwa, Shahidi amesema kwamba wanatoa matangazo na walalamikaji walifahamu utaratibu huo na wengi wao hadi sasa huajiriwa wakati wa msimu wa tumbaku.

Shahidi wa pili Rajabu S. Mkumbwa aliyekuwa anafanyia kazi T.T.P.C. alisema kuwa T.T.P.C. ilivunjwa na Serikali na kutolewa katika Government Notice No. 24 ya 7/2/1986. Baada ya hapo, kuliundwa Bodi ya Tumbaku ikiunganisha shughuli za T.A.T. na T.T.P.C.

Meneja Mkuu alipelekewa agizo la serikali na Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo na Maendeleo ya Mifugo kwa barua ya tarehe 20/4/84 ya kuwa Mamlaka ya Tumbaku na Tanzania Tobacco Processing Company vitavunjwa na pataundwa Bodi ya Tumbaku (Tanzania Tobacco Board) ambayo itahusika na ununuzi wa tumbaku kutoka vyama vya ushirika, kusindika na kuiuza tumbaku yote nchini na nchi za nje. Agizo hilo limetolewa kielelezo $D._1$ na katika hilo agizo, ilitakiwa wafanyakazi wapunguzwe kutoka 1,131 hadi 366. Wafanyakazi 169 kati ya hawa 366 wawe kiwandani.

Ili kutekeleza agizo la Serikali, kuliitishwa kikao cha pamoja cha bodi za Wakurugenzi wa T.A.T. na T.T.P.C. cha 3/1/85 ambapo A. N. Mwakingwe, Mwenyekiti wa tawi la JUWATA T.T.P.C. alihudhuria. Kielelezo $D._2$ kinajieleza na hakikupingwa kutolewa mahakamani kwa upande wa menejimenti. Kikao hicho cha tarehe 3/1/85 kiliongelea mambo mawili muhimu, kukiwa na uanzishaji wa Bodi ya tumbaku na upunguzwaji wa wafanyakazi.

Kielelezo kingine, $D._3$ kinaonyesha kikao cha pamoja cha menejimenti na halmashauri ya JUWATA cha tarehe 23/2/85 ili kuiadili watumishi waliopendekezwa na wasiopendekezwa kuajiriwa katika bodi ya Tumbaku Tanzania. Katika kikao hicho tawi la JUWATA liliwakilishwa na halmashauri nzima, wakiwemo:—

1.	A.N. Mwakingwe	— Mwenyekiti.
2.	M.B. Mabonye	— Katibu Juwata.
3.	A.A. Simchimbey	— Mjumbe Juwata.
4.	T.E. Mtandi	— Mjumbe Juwata.
5.	S. Sekaila	— Mjumbe Juwata.
6.	Waziri Rajabu	— Mjumbe Juwata.
7.	Abdallah Nekaheka	— Mjumbe Juwata.
8.	R. Rangimoto	— Mjumbe Juwata.
9.	Bakari Athumani	— Mjumbe Juwata.
10.	B. Mbunda	— Mjumbe Juwata.
11.	Rashidi Tombo	— Mjumbe Juwata.

Kikao hicho kilichambua kwa kina wafanyakazi kwa kutilia maanani mkataba wa hiari na kuwa Cosmas Haule alikuwa hana sifa za uhasibu kama wengine walioachwa, Lazaro Mizambwa, mlinzi alikuwa hana mafunzo yoyote yale ya ulinzi; Masieba na Cassian Benedict, Wahasibu Wasaidizi, mmoja akiwa hana nafasi na mwenzake kutokuwa na sifa kama wengine. Rajabu Abdallah, fundi seremala idara hiyo ilifutwa; Laban Manda aliomba apunguzwe; Michael Thomas alikuwa amehamishiwa katika chama cha kuweka na kukopa ingawaje hapo awali alikuwa "Fork lift driver".

Baada ya kikao hicho cha tarehe 23/2/85 kilichochambua majina na kupeleka kwenye Bodi, kulitokea mapendekezo mengine ya kuongeza ajira kutoka ile ya kwanza ya 366 hadi kufikia wafanyakazi 500. Ongezeko hili lilifanywa baada ya kujua kuwa vyama vya ushirika havikuwa tayari kuendesha shughuli za tumbaku wakati ule; hivyo ikama ya watu 366 isingetosha kushughulikia zao hilo la tumbaku. Kati ya wafanyakazi 134 waliotakiwa kuongezewa, kiwanda cha tumbaku walipewa 30 tu. Hivyo JUWATA na menejimenti walichambua tena wafanyakazi 30 kati ya wale waliopendekezwa kupunguzwa. Kikao hicho ni cha tarehe 7/3/85. Ushahidi ulipokelewa kama kielelezo $D._5$.

Ili kuthibitisha kuwa baada ya zoezi hili ajira zingine zilikuwa ni za mikataba au msimu, barua mbili za Hadija Ramadhani na Renatus Ngonyani zilitolewa vielelezo $D._6$ na $D._7$.

Hadija ni mfanyakazi wa msimu wakati Renatus aliajiriwa kwa mkataba wa mwezi.

Lalamiko la kuwa wafanyakazi wa T.A.T. walichukua nafasi ya wafanyakazi T.T.C.P. ilikuwa sio kweli kwani ilipoonekana katika kikao cha tarehe 26—28 Februari, 1985 kuwa vyama vya ushirika havikuwa tayari bado kwa kazi ya tumbaku vijijini, T.A.T. waliongezewa wafanyakazi 104 wakati T.T.P.C. waliongezewa wale 30 tu. Ushahidi umeonyesha pia kuwa Mrema na Saidi walihamishwa kutoka Dar es Salaam na kwenda Morogoro pamoja na "fork lift" zao. Barua zao za uhamisho ni vielelezo $D._8$ kwa pamoja. Ni mtu mmoja tu, Ramadhani Changanda aliyeajiriwa kwa upya kwa amri ya bodi ili kuimarisha karakana ya magari. Hakuna hata mlalamikaji mmoja aliyekuwa na sifa za Ramadhani za ufundi wa magari na ilikuwa lazima kuwe na fundi wa magari ili kupunguza gharama na kuongeza ufanisi.

Dai kubwa la JUWATA lilivyo ni kuwa mkataba wa hiari haukufuatwa katika utekelezaji wa agizo. Katika mkataba huu vitu vilivyopakiwa ni kufuata utaratibu wa FILO na pia kutoajiri wafanyakazi wengine kabla ya wale waliostaafishwa. Ushahidi umetolewa wa kutosha kuwa hakuna mfanyakazi aliyeajiriwa isipokuwa Ramadhani, ambaye ni fundi magari na nafasi yake hiyo hakuna hata mmoja wa wale walioachishwa aliyekuwa na ujuzi huo wa ufundi magari. Jambo la kuangalia kwa makini ni hilo la FILO kwani tawi la JUWATA lilishiriki katika uchambuzi wa waliopunguzwa kama sheria ya Usalama kazini kifungu Na. 6(1)(g) ambacho kinataka JUWATA iwasiliane kwanza na menejimenti kabla ya kupunguza ajira na pili utekelezaji wa mkataba wa hiari kama upo kuhusiana na kustaafisha wafanyakazi.

Ushahidi umeridhisha kuwa T.A.T. na T.T.P.C. zote zilivunjwa na Serikali na hatimaye kuunda bodi ya tumbaku yenye wafanyakazi 500. Kuvunjwa kwa vyombo hivyo kulisababisha upunguzaji wa ajira ili kuleta ufanisi zaidi schemu ya kazi. Bodi iliajiri wafanyakazi wachache zaidi kuliko ilivyokuwa mamlaka na viwanda mbali mbali.

Katika sheria hiyo ya Usalama Kazini, inataja utekelezaji wa mkataba wa hiari, na mkataba wa hiari umetaja katika kifungu Na. 7 kuwa kukitokea upunguzaji wa ajira, ni lazima FILO itumike. Mkataba huo kama nilivyonukuu kifungu cha 7 hapo juu hauelezi zaidi ya hapo. Hata hivyo, kesi ya Mahakama ya Rufaa, "Civil Appeal Na. 36. of 1987" kati ya KIHANIRA KULUNGE KIBAYA Vs UNITED AFRICA COMPANY OF TANZANIA LIMITED imetoa ufafanuzi zaidi. Hivyo katika ukurasa wa nne wa hukumu hiyo, mahakama ilisema:

> "The reason given for terminating appellant's employment practice in this country, redundancy is governed by, inter alia, the rule of "FILO" that is First In Last Out. Under this rule, the first person to loose his job in redundancy exercise is the empoyee who has been in employement for the shortest period in the sector concerned. Those who have been with the firm for the longest period are the last people to loose their jobs, in any given section of work unless there are good reasons justifying a departure from the general rule."

Kesi niliyoitaja hapa juu inatujulisha kuwa katika eneo la kazi, kuna idara mbali mbali na wakati wa zoezi la kustaafisha wafanyakazi, wale wa zamani ndio watakaokuwa wa mwisho kutoka. Hii ni katika kila idara na sio kwa kiwanda au kampuni kwa ujumla. Hii inachukuliwa tena kuwa mambo yote ni sawa kati ya wale wafanyakazi. Hata hivyo kunawezekana kuwe na sababu za kuridhisha za kuweza kuacha kufuata huu utaratibu.

Kiongozi wa mgogoro huu ndugu Haule aliajiriwa hapo Tumbaku 1/4/1968 na cheo cha "Assistant Leaf Stastician" wakati anastaafishwa na kuwa kampuni ilimpeleka kusoma masomo ya jioni lakini hakufaulu. Yeye Haule alisema kuwa hakupata mishahara. Kutoa mishahara sio sababu ya kutofaulu mtihani na kupata cheti. DW.2 alieleza kuwa Haule hakuwa na sifa za uhasibu kama wale wengine walioachwa katika idara yake ya uhasibu. Hii ndio sababu ya kumwondoa na kuacha wengine. Wafanyakazi wengine wa zamani nao aidha idara zao zilifutwa kabisa au hawakuwa na sifa zinazotakiwa katika hile idara. Hayo maelezo yanakidhi matakwa ya kesi ya Mahakama ya Rufaa niliyoitaja hapo juu kuwa ni wakati gani inapowezekana kumpunguza kazi mfanyakazi aliye ajiriwa kwanza na ukaacha yule aliyeajiriwa nyuma yake. Maelezo hayo yalikuwa yanakidhi haja na nia ya zoezi lenyewe la kupunguza ajira na kuongeza ufanisi. Wale wachache walioachwa walionekana kuwa watafanya kazi zaidi na kwa ufanisi zaidi licha ya uchache wao kuliko wakiwa wengi na shughuli ile ile. Kama basi hivyo ndivyo ilivyokuwa, basi upunguzaji wa ajira katika kampuni hiyo ya Tumbaku ulifanyika kufuatana na matakwa ya kifungu Na. 6(1) (g) cha Sheria ya Usalama Kazini Cap. 574 inayotawala maswala ya kustaafisha wafanyakazi mahali pa kazi.

Kutokana na uchunguzi uliofanywa na Mahakama ya Kazi na taarifa niliyoletewa, nimeridhika kabisa kuwa Ndugu Haule na wenzake walipunguzwa kazi na sio kuachishwa. Pili kuwa taratibu zote za kisheria zilizingatiwa katika utekelezaji wa zoezi hili na mwisho kuwa hakuna maswala yoyote ya kisheria yaliyojitokeza walitekeleza agizo la Serikali la kupunguza ajira na kuongeza ufanisi kama ilivyotakiwa. Madai ya walalamikaji yamefutwa na kuhalalisha uamuzi wa menejimenti.

Uamuzi huu umetolewa nami na kushuhudiwa na mkono wangu leo hapa Dar es Salaam siku ya Jumatano tarehe 29 mwezi Novemba 1989.

Coram:

Ndugu A.R. Manento — Naibu Mwenyekiti.
Ndugu F.N. Kitana — Mshauri (ATE).

Dar es Salaam,
29 Novemba, 1989

J. C. RWEGASIRA.
Waziri wa Kazi, Utamaduni na Ustawi wa Jamii

TUZO

TUZO hii imetolewa nami na kushuhudiwa na Muhuri wa Mahakama ya Kazi leo hapa Morogoro siku ya Jumamosi tarehe 16 Desemba, 1989 na inakuwa na nguvu za sheria mara moja.

A. R. MANENTO,
Naibu Mwenyekiti Mahakama ya Kazi

Certified true copy of the original.

B. E. NYAMUBI,
Registrar

TAARIFA YA KAWAIDA NA.195

MAHAKAMA YA KAZI

UCHUNGUZI WA MGOGORO WA KIKAZI NA. 55/1987/88

baina ya

JUMUIYA YA WAFANYAKAZI TANZANIA—JUWATA

(Kny: F..F. Mkwavi)

na

KILIMANJARO TEXTILE CORPORATION

UAMUZI

Ndugu Fedelis Francis Mkwavi alijiariwa na kiwanda cha Nguo cha hapa Dar es Salaam kijulikanacho kwa jina la Kilimanjaro Textile (KILTEX) mnamo tarehe 1/4/1974 baada ya kuhamishiwa kutoka Mwanza Textile Ltd. (MWATEX). Aliajiriwa kwa cheo cha dying and Finishing Officer'. Ndugu Mkwavi alionyesha bidii ya kazi na kumudu kazi zake na akawa anapandishwa vyeo hadi kufikia 'Mill Manager' hapo tarehe 12/3/86. Siyo hilo tu, bali aliwahi kuwa Kaimu Mmeja Mkuu, akimiliki viwanda viwili vya KILTEX, kile cha Arusha na hiki cha Dar es Salaam. Shangwe hiyo haikuendelea sana, kwani tarehe 31/1/1987 Ndugu Mkwavi aliachishwa kazi.

Hakuridhika na hatua hiyo ya kuachishwa kazi. Alilalamika katika vyombo mbalimbali, vikiwemo pamoja na Ikulu. Juwata ambayo ilifikisha suala hili kwa Kamishna wa Kazi na hatimaye likafika kwangu. Baada ya uchunguzi, niliamuru suala hili lipelekwe Mahakama ya Kazi kwa uchunguzi chini ya kifungu Na. 9A cha Sheria ya Mahakama ya Kazi Na. 41/1967 kama ilivyorekebishwa na sheria Na. 18/1977 ili baada ya uchunguzi, niletewe taarifa ili nitoe uamuzi chini ya kifungu Na. 9B cha sheria hiyo hiyo. Uchunguzi umefanywa na nimeletewa taarifa na huu ndiyo uamuzi wangu.

Katika uchunguzi uliofanyika imeonyesha kwamba KILTEX ina viwanda viwili, kimoja kikiwa hapa Dar es Salaam na kinginc huko Arusha. Viwanda hivi kila kimoja kina kiongozi wake ajulikanaye kama 'Mill Manager' na juu yao, kuna Meneja Mkuu na 'Technical Manager' ambaye huangalia mambo ya kiufundi ya viwanda vyote viwili. Huyu pamoja na wale 'Mill Managers' wawili wanawajibika kwa Meneja Mkuu. Kabla ya mgogoro huu, huyu 'Technical Manager' ofisi yake ilikuwa hapa Dar es Salaam, makao makuu ya Kampuni na shughuli za kiufundi za kila siku huwa zikifanywa na mafundi chini yake huko huko viwandani. Mishahara na malupulupu mengine ya "Mill Manager" na "Technical Manager" yalikuwa sawa sawa. Wote watatu wakiwajibika kwa Meneja Mkuu ambaye ofisi yake iko hapa Dar es Salaam.

Uchunguzi umeonyesha kuwa mgogoro huu ulianza tarehe 15/4/1986 alipoletwa Meneja Mkuu wa KILTEX ambaye hakuwa mtanzania. Huyu alikuwa mgeni kutoka Pakistani na alikuwa anaitwa Akthar. Kukutana kwa mlalamikaji na aliyekuwa awe mkuu wake wa kazi kunaonyesha kutofurahi kwa mlalamikaji au kutomtambua mara moja. Nimefikia uamuzi wa kuamini hivyo kwa maneno ya mlalamikaji mwenyewe alivyosema Mahakamani kama ifuatavyo:

> "Nilimwomba Akthar anipishe kwenye kiti niweze kumkabidhi na aliniambia nisitie wasiwasi bali nichukue vitu vyangu na tutaelezana kesho yake".

Baada ya mlalamikaji kutambulishwa kuwa huyo Akthar ndiye aliyekuwa Meneja Mkuu, madaraka yake ya kukaimu yalikuwa yamekwisha hapo hapo na yeye Akthar ndiye aliyestahili zaidi kukaa katika kiti hicho na meza hiyo kuliko mlalamikaji.

Wafanyakazi wa KILTEX Dar es Salaam hawakutaka Akthar aajiriwe na TEXCO kwa cheo hicho cha Meneja Mkuu kwani walipinga ajira hiyo mbele ya Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi na hata mbele ya Waziri mdogo, Wizara ya Viwanda na Biashara. Inaonyesha kuwa Bodi ya Kiltex iliamini kuwa mlalamikaji hakuwa naushirikiano nao na alihamishiwa katika kiwanda cha nyuzi kilichoko huko Ubungo, Mjini Dar es Salaam. Uhamisho huo ulifutwa baada ya mlalamikaji kutoa sababu za kuridhisha kuwa hakutaka kuhamia katika kiwanda hicho kama Meneja Uzalishaji. Sababu alizozitoa ni mbili kuwa hakuwa na ujuzi wa kazi hizo na pili kuwa yeye aliajiriwa na Kiltex hivyo asingelihamishiwa na TEXCO kwenda katika kiwanda cha nyuzi Ubungo ambacho kilikuwa na Bodi yake ya Wakurugenzi. Menejimenti walitoa ushahidi kuwa ujuzi aliokuwa nao mlalamikaji wa shughuli za uzalishaji nguo nauzoefu wake, alikuwa ndiye mtu aliyefaa zaidi kushika nafasi hiyo ya Meneja Uzalishaji katika kiwanda cha nyuzi.

Baada ya Akthar kuwa kazini, mlalamikaji hakupenda uongozi wake kwani alidai katika ushahidi kuwa Meneja Mkuu huyo alitaka yeye mlalamikaji afuate tu jinsi Meneja Mkuu alivyotaka kuendesha kiwanda. Pia alikuwa haridhiki na tabia ya Meneja Mkuu kutembelea kiwanda yeye mwenyewe bila kumuarifu kwanza mlalamikaji. aliyekuwa "Mill Manager". Mambo yote hayo mawili yalikuwa chini ya uamuzi na matakwa ya Meneja Mkuu hata bila kushauriana na mlalamikaji. Siyo yeye aliyetakiwa kumkosoa Meneja Mkuu wake bali alitakiwa kutekeleza yale aliyotaka Meneja Mkuu mradi tu hayakuwa kinyume na sheria za nchi au taratibu za kazi na usalama wa kiwanda.

Baada ya siku kupita. bodi ya Kiltex iliamua kumhamisha mlalamikaji. Uhamisho huo ni wa vitu viwili, kwanza kubadilishwa kazi na cheo. kutoka kuwa "Mill Manager" na kuwa "technical Manager". Pili ni kuhamia Kiltex Arusha. Uhamisho huo uko katika barua ya uhamisho iliyotolewa kielelezo P.30 ambayo ilielezea zaidi kuwa uhamisho huo ulitolewa na Bodi ya Wakurugenzi katika kikao chake cha 48. Uhamisho huo ulikuwa wa mara moja. Barua ya uhamisho ni ya tarehe 10/10/1986. uhamisho huu ndiyo chimbuko la mgogoro huu kwani mlalamikaji alikataa uhamisho na hatimaye kuachishwa kazi.

Kutokana na kutoridhika na uhamisho huo, mlalamikaji aliiandikia Bodi barua na pia kuomba apewe nafasi ya kujieleza kwa nini hataki huo uhamisho. Ombi lake lilikubaliwa na tarehe 3/1/87 alijieleza mbele ya Bodi ya Wakurugenzi. Kwa maneno ya mlalamikaji mwenyewe, alisema Bodi ilimfafanulia nia na madhumuni ya huo uhamisho kwa maneno yafuatayo:—

> "Niliambiwa kuwa Bodi peke yake ndiyo iliyotoa uamuzi huo bila kushirikishwa menejimenti kutokana na uzoefu wa muda mrefu. Sababu Arusha kuna mitambo mipya, Bodi imeona nihamie Arusha kwa sababu ya "close Supervision"
>
> Mwenyekiti aliniambia nilichotakiwa ni uamuzi kuwa nitakwenda Arusha au sitakwenda, ili kuiwezesha Bodi kuchukua hatua za nidhamu. Kama kuna maelezo yoyote yale, nitamweleza ofisini kwake.
>
> Mwenyekiti alinitahadharisha kwamba endapo nitakataa uhamisho Bodi haitasita kuniachisha kazi".

Mlalamikaji alijulishwa uamuzi huo wa Bodi baada ya kutoa sababu zake kuwa hana ujuzi na kazi hiyo mpya. Hata hivyo alipewa muda wa juma moja kufikiria huo uamuzi wa Bodi ili atoe jibu la mwisho, tarehe 15/1/85 alimjulisha Mwenyekiti wa Bodi kuwa amekataa uhamisho na cheo kipya cha "Technical Manager" Baada ya kukataa, Bodi ilitekeleza yale aliyoambiwa ya kuachishwa kazi kama hatua ya nidhamu, na kwa barua kielelezo P.34 ya tarehe 31/1/1987 mlalamikaji Ndugu Mkwavi aliachishwa kazi na sababu za kuachishwa kazi ziliandikwa kwenye hiyo barua.Kwa ufasaha zaidi, nanukuu sehemu muhimu ya P. 34 kama ifuatavyo:

> "However the Board cautioned you and made it very clear to you, that, since the transfer was crucial in-view of what was happening in the company oparationally if you insisted on disobeying the Board's decision on the transfer, it would be viewed as an act of gross misconduct, indiscipline and insurbodination which attracts severe disciplinary measurers including that of summary dismissal".

Sehemu hiyo ya barua ya kuachishwa kazi imetoa kwa muhutasari sababu za kuachishwa kazi kwa mlalamikaji kuwa ni kukataa na kutotii amri ya viongozi wake wa kazi, yaani Bodi ya Wakurugenzi. Hatua ya kuachishwa kazi kwake mlalamikaji haikuwa kitu kigeni au cha kushituliwa kwani mlalamikaji alipoitwa mbele ya Bodi alijulishwa kata kata ni kitu gani kitakachofuata akikataa huo uhamisho.

Uchunguzi umeonyesha kuwa hapakuwa na sababu yoyote ya kusema kuwa mlalamikaji hakupewa shitaka wakati alipewa uhamisho na kukataa, akijitetea kwa maandishi na kwa mdomo mbele ya Bodi kuhusu swala hilo hilo la uhamisho. Madai hayo hayana msingi wowote ule wa kisheria au kiutaratibu. Pili swala la kuwa yeye mlalamikaji hakuwa mtaalam na mtaalam Ndugu Sagatwa aliachwa nalo siwezi kulikubali ili kuhalalisha kitendo cha mlalamikaji. Kukubali hivyo ni sawa na kukubali kuwa Bodi haikuwa na madaraka juu yake na ni yeye alikuwa apangie Bodi. Bodi ndiyo

iliyokuwa inajua ufanisi wa wafanyakazi wake na ilijua ni nani anaweza kufanya kazi gani na nani hawezi. Mlalamikaji aliwajibika kufuata amri ya mwajiri wake kwani ilikuwa halali. Nakubaliana na mlalamikaji kuwa ni kweli hakuwa na sifa za kuwa "Technical Manager" lakini pia hakuwa na sifa za kuwa "Mill Manager". Kule kupewa cheo hicho cha Mill Manager" kunaonyesha kuwa Bodi ilikuwa na uwezo wa kumpa mfanyakazi cheo ambacho hana sifa zake mradi tu wameridhika kuwa ataweza kumudu hizo shughuli.

Ningependa kuchukua nafasi hii kueleza kuwa maswali ya kupandisha wafanyakazi vyeo sio ya JUWATA wala ya uhamisho. Menejimenti haikutakiwa kushauriana na JUWATA katika kumhamisha mlalamikaji, kutoka KILTEX Dar es Salaam na kumpeleka KILTEX Arusha. Ushaidi wa PW2 Mwenyekiti wa Tawi la JUWATA umetolewa mahali ambapo siyo kwake na hauna uzito wowote ule katika mgogoro huu.

Uchunguzi umeonyesha kwamba sababu hasa zilizosababisha mwajiri kumwachisha kazi mlalamikaji ni kitendo cha mlalamikaji cha kukataa uhamisho wa kutoka katika cheo cha "Mill Manager" nakuwa "Technical Manager" huko Arusha. Sababu za kumbadilisha cheo hicho zimeelezewa na mwajiri kuwa ni kutokana na uzoefu wake wa siku nyingi na ujuzi katika shughuli za nguo hivyo kwamba Bodi kumwona kuwa ataweza kuangalia na kusimamia kwa karibu zaidi mitambo mipya ya kiwanda cha nguo "KILTEX ARUSHA" ambacho ndiyo "roho" ya KILTEX kwa jumla. Pamoja na kuwa alikuwa hana sifa za "Technical Manager", Menejiment waliona kuwa hawakuwa na mfanyakazi mwingine mwenye uwezo huo katika kiwanda hicho. Kwa sababu ya uangalizi wa karibu, ofisi ya "Technical Manager" ilihamishiwa Arusha badala ya kuwa hapa Dar es Salaam, mbali na mitambo yenyewe.

Bodi ya Wakurugenzi ndiyo iliyokuwa na mamlaka katika kiwanda cha nguo "KILTEX" na pili kuwa Bodi hiyo hiyo ndiyo yenye mamlaka ya kumhamisha na kumbadilisha kazi mfanyakazi wa KILTEX kama inaona kuwa kumfanya hivyo ni kwa faida ya kiwanda. Hivyo basi, mlalamikaji aliwajibika kwa Bodi ya Wakurugenzi na siyo kinyume chake.

Kitendo cha mlalamikaji cha kukataa uhamisho kwa kuamini kuwa Bodi ilikosea kufanya hivyo kutokana na kutoelewana kwake na Meneja Mkuu wake Akthar ni kitendo cha utovu wa nidhamu, kitendo hicho kinaitwa kwa kiingereza "insurbonation" ambacho adhabu yake ni kufukuzwa kazi kutokana na nyongeza ya pili, kifungu 'K' cha sheria ya Usalama Kazini. Mlalamikaji alitakiwa kutii hilo agizo na kama angelishindwa hiyo kazi, mwajiri wake angelijua aidha kwa kumwona utendaji wake au kwa malalamiko ya mlalamikaji kuwa ameshindwa kazi. Nasema hivyo kwa sababu Bodi inasema kuwa yeye ndiye waliyemwona kuwa anafaa kwakazi hiyo kuliko mtu mwingine yeyote yule na mlalamikaji alijulishwa hivyo na alirudia kusema hivyo katika ushahidi wake. Kukataa moja kwa moja ni kitendo cha dharau ambacho hakiwezi kuvumiliwa kwani kikivumiliwa kitavuruga mtiririko mzima wa madaraka mahali pa kazi.

Baada ya kupewa barua ya uhamisho kwenda Arusha kuwa "Technical Manager" mlalamikaji alikataa kwa maandishi na kutoa sababu zake. Bodi ya Wakurugenzi ilikaa nakujadili sababu hizo, haikutosha mlalamikaji akaitwa mbele ya Bodi, akajieleza tena nakujulishwa msimamo wa Bodi naye akashikilia msimamo wake wa kukataa na akatahadharishwa hatua itakayochukuliwa dhidi yake kama ataendelea kukataa uhamisho huo. Alipewa muda wa juma moja ili afikirie tena na hatimaye amjulishe Mwenyekiti wa Bodi uamuzi wake wa mwisho. Hata baada ya muda huo, alikataa uhamisho na ndipo alipoachishwa kazi kwa huruma za Bodi badala ya kufukuzwa kwa kitendo cha utovu wa nidhamu na kutotii maamuzi ya Bodi ya Wakurugenzi. Hakuna kitu chochote kile alichofichwa na Bodi na baada ya hatua hiyo ya nidhamu kuchukuliwa ameanza tena kulalamika kwa kitu alichokuwa anajua au ana sababu za kujua kuwa kitatokea. Ikiwa basi mlalamikaji alipewa nafasi ya kujitetea mbele ya Bodi, licha ya utetezi wake wa awali kwa barua kabla hajapewa nafasi hiyo rasmi, sioni kuwa kuna taratibu ambazo hazikufuatwa. Alipewa nafasi ya kujitetea mbele ya mamlaka yake ya ajira, yaani Bodi ya Wakurugenzi.

Mwisho kabisa napenda kueleza kuwa sababu zilizoacha Ndugu Mkwavi aachishwe kazi ni utovu wa nidhamu kwa kukataa amri halali ya Bodi ya Wakurugenzi ya uhamisho kutoka KILTEX Dar es Salaam na kwenda KILTEX Arusha kwa cheo cha "Technical Manager" ambacho kiko sambamba na cheo cha "Mill Manager" alichokuwa nacho hapa Kiltex Dar es Salaam. Taratibu zote za kisheria zilifuatwa na mwajiri walipoamua kumwachisha kazi mlalamikaji, na kuwa hakuna masuala mengine yeyote yale ya kisheria yaliyojitokeza. Baada ya kusema yote hayo, nakubaliana na uamuzi wa Bodi ya Wakurugenzi na ninafuta madai ya mlalamikaji. Aliachishwa kazi kwa uhalali kabisa.

Uamuzi huu umetolewa nami na kushuhudiwa na mkono wangu leo hapa Dar es Salaam siku ya Jumatatu tarehe 11 mwezi wa Septemba, 1989.

Coram: C. T. KISANJI,
Waziri wa Kazi, Utamaduni na Ustawi wa Jamii

A. R. MANENTO,
Naibu Mwenyekiti

TUZO

TUZO hili imetolewa nami na kushuhudiwa na Muhuri wa Mahakama ya Kazi leo hapa Dar es Salaam siku ya Ijumaa tarehe 22/9/89 na inakuwa na nguvu za sheria mara moja.

A. R. MANENTO,
Naibu Mwenyekiti Mahakama ya Kazi

Certified true Copy of the Original

B. E. NYAMUBI,
Registrar

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 196

MAHAKAMA YA KAZI

UCHUNGUZI WA MGOGORO WA KIKAZI NA. 42 WA 1987/88

baina ya

HUSSEIN KAUTIPE—TANGA

na

KWAMKORO TEA ESTATE LTD.—TANGA
(Mwajiri)

UAMUZI

Malalamiko ya mgogoro huu yalifikishwa mbele ya aliyekuwa Waziri kabla yangu, naye akaagiza kupitia kwa Katibu wake yapelekwe mbele ya Kamishna wa Kazi.

Kamishna wa Kazi alipitia kumbukumbu zote, akaona huu ni mgogoro ambao ungeweza kuchunguzwa chini ya fungu la 9A la Sheria ya Mahakama ya Kazi. Kwa hiyo aliomba kibali cha Waziri ili mgogoro huo upelekwe mbele ya Mahakama ya Kazi. Mgogoro ulifikishwa mbele ya Mahakama ya Kazi mwezi Januari, 1988.

Kwa sababu mbali mbali ikiwa ni pamoja na kubadili washauri nyakati mbali mbali na kuchelewa kuomba ruhusa ya kutetewa na wakili, mgogoro ulianza kuchunguzwa na kumalizika 2/9/89.

Historia ya mgogoro huu inayonyesha mlalamikaji Kautipe aliajiriwa hapo tarehe 31/8/64 na Kimamba Fibres. Mwaka 1967 shamba la Kimamba likawa moja ya mashamba yaliyotaifishwa. Baada ya mashamba kutaifishwa yeye alibaki pale Kimamba Fibres akishughulikia uhasibu mpaka 1969 alipohamishiwa Makao Makuu ya Shirika la Mkonge hapo 1969 na akapewa kazi ya kusafirisha kwa meli (Shipping) mpaka 1971. Kutoka 1971—1983 alihamishiwa mashamba mbali mbali. Tunaamini ajira yake kuanzia mashamba yalipotaifishwa mpaka 1983 ilihifadhiwa katika mashirika/ mashamba alipokuwa akihamishiwa ikiwa ni pamoja na Shirika la Mkonge lililokuwa Shirika mama la mashamba yaliyotaifishwa. Mlalamikaji alikuwa anapewa nafasi mbali mbali katika mashamba hayo ikiwa ni pamoja na kuwa Meneja na Mhasibu. Alipostaafishwa mwaka 1983 alikuwa na cheo cha mhasibu msaidizi.

Vielelezo 11 vililetwa kuthibitisha malalamiko yalivyokuwa. Kufuatana na kielelezo $P._1$ mlalamikaji Kautipe alipokea barua yenye kumbukumbu Na. MU/08/1 ya tarehe 16/3/83. Barua hii ilikuwa na kichwa cha habari kama ifuatavyo "TAARIFA YA MWEZI MMOJA KUSTAAFU KAZI NDG. H. KAUTIPE MHASIBU MSAIDIZI." Barua hiyo ilitoka kwa Meneja Mkuu, Kampuni ya Mashamba ya Chai Kwamkoro (KWAMKORO TEA ESTATES LTD.) Barua hiyo inaeleza sababu za kustaafu kwa maneno yafuatayo nanukuu:

"SIRI"

"KWAMKORO TEA ESTATES CO. LTD.

Our Ref. MU/08/1 Date: 16th March, 1983

Ndugu Hossein K. Hossein,
Mhasibu Msaidizi,
Kampuni ya Mashamba ya Chai,
KWAMKORO.

TAARIFA YA MWEZI MMOJA KUSTAAFU KAZI NDUGU H. KAUTIPE—MHASIBU MSAIDIZI

Tangu kuundwa kwa Kampuni, ulitoa ombi la kuhamishwa kwenda sehemu nyingine au kuruhusiwa kustaafu. Menejimenti iliomba kuwepo kwako kusaidia kama Mhasibu Msaidizi kazi ambayo imebainika hukuipenda mpaka sasa.

Baada ya kipindi kirefu kumekuwa na tatizo kwenye Idara. Imebidi kikao cha viongozi wa Chama, JUWATA na Idara kukutana kuangalia kwa undani zaidi matatizo ya Wafanyakazi wa Kampuni, Idara ya fedha na wewe mwenyewe.

Kikao kimetoa azimio kwa kuomba Menejimenti ikubali ombi lako la kustaafu. Hivyo kwa barua hii unaruhusiwa kuchukua likizo yako na kupumzika iwe kama Notisi yako ya mwezi mmoja wakati malipo yako ya uzeeni yanatayarishwa huko Makao ya Mamlaka ya Mkonge Tanga. Unaweza kuanza kupumzika kuanzia 20/3/1983—16/4/1983.

Hii itakuwa baada ya malipo na wewe kumaliza posting voucher zako kwenye Cash Books zote tatu. Main, Kibarua, Stores Purchases. Utatakiwa kukabidhi baki ya fedha, Cash Books na mali nyinginezo kwa Meneja Mkuu. Pia hesabu za W.F.P. na Depositi A/C ziwe kamili.

Kwa niaba ya Mamlaka ya Mkonge na Kampuni ya Kwamkoro, Menejimenti, na Wafanyakazi tunakutakia kila la heri.

Ahsante sana
KAMPUNI YA MASHAMBA YA CHAI KWAMKORO

Sgn. Meneja Mkuu

Nakala: Meneja Mkuu,
Mamlaka ya Mkonge Tanzania,
TANGA.
Wenyeviti—CCM, Ndola Kwamkoro na Ngua)
Utekelezaji wa Azimio la Kikao cha Viongozi wa Chama JUWATA na Wakuu wa Idara 15/3/83".
Mwenyekiti—JUWATA Kwamkoro

Baada ya kustakabadhi barua na kuisoma alishangaa kwa yale aliyoyasoma kwa kuwa hakuelewa imekuwaje anasemekana aliomba kustaafu wakati hakuwa ameomba hivyo. Alipewa hata kumbukumbu za kikao ambazo alizitoa kama kielelezo $P._2$. Kwa kuwa alifikiri kikao kilichomjadili hakikuwa halali alikwenda kumwona Mwenyekiti wa Bodi ambayo alimwambia angalishughulikia jambo hili. Lakini muda ulipopita alimwandikia barua ya kukumbushia. Alizitoa barua alizomwandikia Mwenyekiti kama kielelezo $P._{3A}$ na $P._{3B}$. Kwa kuwa muda mrefu alikwenda Makao Makuu JUWATA na wakampa barua aanzie ngazi ya chini. Barua ya Makao Makuu ya JUWATA aliipeleka Mkoani na Mkoa ukaandikia Katibu wa Tawi la JUWATA Mahali pa kazi. Baada ya barua mbali mbali kati ya JUWATA katika ngazi mbali mbali mwishowe alienda kumwona Waziri. Waziri alimwandikia Kamishna wa Kazi na mwishowe Kamishna wa Kazi aliuleta mgogoro huu kwenye Mahakama ya Kazi. Mlalamikaji anaomba kurudishwa kazini bila kupoteza haki zake.

Mwisho wa ushahidi wa mlalamikaji ulipofikiwa, wakili Muhula kwa ajili ya walalamikiwa alimleta Bwana Stanley Jacob Isanzu ambaye ndiye aliyeanza kuwakilisha Kampuni kabla ya kumleta Wakili Muhula, kama shahidi wao wa kwanza ($DW._1$). Yeye alisema kwamba anafahamu kutokana na kumbukumbu kwamba Nd. Kautipe aliwahi kufanya kazi katika shamba la Kwamkoro Sisal Estates; kwamba Kwamkoro Sisal Estates, kama kampuni haipo tena. Sababu ni kuwa shamba hilo au kampuni kwa jina hilo ilikuwa chini ya Mamlaka ya Mkonge (T.S.A.) mpaka 1987 na ilihamishiwa Mamlaka ya Chai (Tea Authority) kwa kuwa ilikuwa inashughulikia chai.

Mwaka 1988 kampuni hiyo ilichukuliwa na kampuni iliyoundwa kati ya Mamlaka ya Chai na Shirika la Maendeleo la Jumuia ya Madola, Mamlaka ikiwa na asilimia arobaini ya hisa na nyingine asilimia sitini zikiwa ni za Shirika la Maendeleo la Jumuiya ya Madola.

Kampuni ilichukuliwa pamoja na mali na madeni (assets na liabilities). Alisema aligundua kwamba mlalamikaji aliajiriwa na Kwamkoro Estates. Aligundua mlalamikaji aliachishwa kazi mwaka 1983 kwa haki na kisheria, kwa kuwa kulikuwa na kikao cha tarehe 15/3/83 cha uajiri ambacho washiriki wake ni wakuu wa Idara na Mwenyekiti akiwa ni Meneja Mkuu. Vile vile mwenyekiti wa CCM na Mwenyekiti wa JUWATA walikuwepo kama wajumbe. Alisema hawa ndio wanaohusika na nidhamu.

Isanzu aliendelea kueleza kuwa Kautipe hakuridhisha Kamati kwa kazi zake na kwa hiyo kamati iliona afukuzwe kazi au akubali kustaafu. Alisema Kautipe aliitwa mbele ya kikao akahojiwa na baada ya kuhojiwa akakubali kustaafu na

:wa hiyo akaandikiwa barua na kulipwa haki zake na alilipwa -iaye akapokea. Kufuatana na utaratibu alisema Isanzu, kama -iakuridhika angekwenda kwenye tawi la JUWATA :ulalamika kuhusu kutoridhika lakini Kautipe hakufanya -iivyo. Ikumbukwe Isanzu hakuwapo wakati Kautipe -naachishwa kazi.

Katika kujibu masuala yaliyoulizwa na Kautipe alisema yeye -ni Afisa Mwendeshaji na mashauri yote ya wafanyakazi yako -nikononi mwake. Isanzu aliendelea kueleza kwamba :ufuatana na taratibu za SCOPO Meneja Mkuu anaweza :uajiri kutoka MSU. 1 mpaka MSU. 3; Kamati ya Uajiri naweza kuajiri kutoka MSU. 4 mpaka MSU. 5; Bodi ya Wakurugenzi inaweza kuajiri kuanzia MSU. 6 mpaka MSU. 14. Alisema mlalamikaji alikuwa MSU. 5. Alisema mlalamikaji hakuajiriwa na Bodi. Mwaka 1983 mshahara wa MSU. 5 ulianzia Sh. 2,010/-.

Katika kujibu masuala ya Muhula, Wakili, kwa ajili ya walalamikiwa Isanzu alithibitisha kwamba kilikuwepo kikao kilichoongelea kuhusu hoja kwamba Kautipe afukuzwe au astaafu. Kwa azimio la kikao, alisema kulikuwapo mwafaka kwamba huyu mlalamikaji aruhusiwe kustaafu. Kumbukumbu za kikao zilitolewa kama kielelezo $D._1$ lakini hiki nisawa na kielelezo $P._2$. Kwa hiyo hazikuwapo sababu za kupokea tena kumbukumbu hizo. Mshauri Msaliboko alimuuliza shahidi -nzu kama kuna barua ya kuomba kustaafu akasema hawezi -pata. Vile vile hajui kama aliarifiwa afike kwenye kikao au hata kama alifika. Alisisitiza kwamba Kamati ya Ajira na nidhamu ndiyo iliyokuwa na mamlaka ya kushughulikia Nd. Kautipe kwa kuwa alikuwa kwenye MSU. 5.

Baada ya pande zote mbili kutoa ushahidi ndipo Mahakama ilipokea hoja za mwisho pamoja na maoni ya mshauri mmoja naye ni Nd. Msaliboko. Ndugu Nyange aliyekuwa mshauri upande wa ATE hayupo kazini tena. Aidha hakuhudhuria vikao vyote na kwa hiyo hakuleta maoni yake.

Kabla hatujaendelea zaidi ni vizuri kutia maanani masuala yaliyotakiwa kuchunguzwa nayo ni:—

(i) Kama Ndugu Kautipe alistaafu kazi kwa hiari yake mwenyewe.

(ii) Masuala mengine yoyote ya kisheria yanayojitokeza katika mgogoro huu.

Kuna ushahidi kwamba tarehe 30 Juni, 1983 mlalamikaji Kautipe alimwandikia Mwenyekiti Mtendaji, Mamlaka ya Mkonge Tanzania akilalamika kwamba ameonewa jinsi -yoachishwa kazi katika barua yenye Kumb. Na. MU/08/1 -a tarehe 16/3/83 iliyoletwa Mahakamani kama kielelezo, $P._1$ na ambayo tumekwishainukuu hapo awali. Baada ya kuona yaliyomo kwenye barua hiyo inatubidi tutupie macho kielelezo $P._2$. Kielelezo $P._2$ ni kumbukumbu za kikao maalum cha dharura cha Wakuu wa Idara pamoja na wenyeviti wa CCM na JUWATA cha tarehe 15/3/1983 kwenye ofisi ya mikutano Makao Makuu ya Kampuni na ikaonekana huyu Kautipe hakuwa na sifa za kuwa mkuu wa Idara ya fedha. Lakini Mamlaka ya Mkonge iliona ni vizuri abaki. Kwa maneno ya kikao "Iliombwa kuwa abaki kama Msaidizi wa Mhasibu Mkuu atakayekuwapo". Kutokana na hilo, Taarifa na mishahara ilichelewa bila sababu. Baadaye alipatikana Mhasibu Mkuu mwingine ambaye alikuwapo na kikao kilikuwa na wasiwasi kwamba angeondoka. Kutokana na kumbukumbu inaelekea yeye Kautipe hakuwa anashirikiana na Wahasibu Wakuu waliokuwa wanaajiriwa. Meneja Mkuu aliyekuwa Mwenyekiti wa kikao Nd. D.M. Mwema alitoa habari kwamba Kautipe aliwahi kuomba uhamisho hapo nyuma na Mamlaka ya Mkonge walikataa. Halafu aliomba kustaafu kwa kuwa umri wake ulikuwa mkubwa na anastahili kustaafu na alikataliwa kwa sababu ya kungoja kukabidhiana na Mhasibu Mkuu atakayeajiriwa. Kwa hiyo kikao kikaamua kwamba ombi lake la kustaafu likubaliwe.

Mlalamikaji anasema kikao hicho cha dharura hakikuwa na uwezo wa kumjadili. Kutokana na barua yake alilalamika kwa Mwenyekiti Mtendaji, Mamlaka ya Mkonge Tanzania kwamba Meneja Mkuu aliita kikao hicho kupika majungu, kumkashifu na kumsaliti mbele ya wafanyakazi wenzake. Kutokana na vielelezo mbali mbali shauri hili lilishughulikiwa na JUWATA katika ngazi mbali mbali na mwisho ikaonekana si kweli kwamba Kautipe aliwahi kuomba kustaafu na kwamba msingi wa kuomba haukuwapo kwa kuwa 1983 alikuwa na miaka 47 tu. Upande wa Menejimenti umesikia maelezo ya Kautipe na kuviona vielelezo mbali mbali lakini hakuna ushahidi ulioletwa kupinga kwamba Kautipe hakuwahi kuomba kwa *mdomo* au *maandishi* kustaafu kama inavyodaiwa katika vielelezo mbali mbali e.g. $P._3$, $P._6$ na $P._7$.

Baada ya kuona maelezo ya ushahidi na vielelezo vilivyoletwa na mlalamikaji sasa tuone ushahidi wa kupinga malalamiko hayo. Nd. Muhula katika maelezo yake ya mwisho (Final Submissions) alisema kwamba kuhusu hoja kama Kautipe alistaafu kwa hiari yake mwenyewe alisema kwamba:—

(a) Madai ya Mlalamikaji ni kwamba alistaafishwa na Mwajiri wake bila yeye kuomba au kwa hiari yake na kwamba kikao kilichozungumzia suala lake hakikuwa halali. Mwajiri amepinga madai hayo kwa kutoa maelezo ya vielelezo. Mahakama imewaona na kuwasikiliza. Ningependa kuiachia Mahakama iamue yenyewe ni ushahidi gani wa pande zote mbili iuamini na imshauri Mheshimiwa Waziri kadiri itakavyoona.

(b) Imedhihirika kutokana na ushahidi wa pande zote mbili kuwa mlalamikaji amekiuka utaratibu wa Kisheria katika kufuatilia haki zake. Hakuna ubishi kwamba yeye ni mwanachama wa JUWATA. Hivyo anabanwa na Sheria iliyoanzisha jumuiya hiyo (No. 24 of 1979). Kifungu cha 7(1) cha sheria hii kinasema:—

The affairs and activities of JUWATA and their conduct and management, shall be governed by the rules. Kanuni ya 53(a) inazungumzia hatua za kutatua mgogoro wa kazi mahali pa kazi kama ifuatavyo:—

> Rule 53(a) Ngazi ya **kwanza** ya kutatua mgogoro baina ya Mwanachama au mwanachama wa JUWATA na Mwajiri ni Kamati ya Tawi ya mahali pake pa kazi kama ipo, au Ofisi ya Wilaya kama mahali hapo hakuna Kamati ya Tawi.
>
> Ni dhahiri kwamba mgogoro wa kikazi lazima upitie ngazi ya chini kabisa, ambayo ni Kamati ya Tawi ili mgogoro utatuliwe katika hali ya amani (Amicable settlement). Na jambo hili linawezekana tu kwa kuanzia ngazi ya chini kabisa.
>
> Ushahidi uliopo unaonyesha kwamba Mlalamikaji hakufuata utaratibu huu wa kisheria. Hivyo mwajiri anaiomba Mahakama kuwa inishauri nizingatie ukweli huu."

Ni kweli Kautipe alipaswa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria. Lakini yeye hakufuata utaratibu huo. Izingatiwe lakini kwamba Kautipe kwanza alilalamika kwa Mwenyekiti Mtendaji. Haieleweki kwa nini baada ya hapo hakwenda kwenye tawi la JUWATA mahali pa kazi.

Mshauri Msaliboko alitoa maoni kwamba hakuna ushahidi kwamba Mlalamikaji aliomba kustaafu, na hangeweza kuomba kustaafu kwa kuwa alikuwa na miaka 47 tu. Yeye anasema baada ya kuangalia ushahidi wote pamoja na kumbukumbu anaona uongozi ulimstaafisha kwa sababu zao kama inavyothibitika katika kielelezo $P._2$ kwamba alikuwa anasababisha wahasibu walioajiriwa wasipende kuendelea na kazi.

Uongozi kutokana na $P._2$ haukumwita Kautipe kujieleza. Baada ya kustaafu Nd. Msaliboko anasema kwamba mlalamikaji ilibidi afuate taratibu ngazi za kutoka Tawi, Wilaya, Mkoa na Makao Makuu.

Ni vizuri tuzingatie kwamba ngazi za juu ziliamuru shauri liangaliwe kutoka tawini. Hii ni kukidhi hoja ya wakili Muhula kwamba sheria inataka mlalamikaji aanzie tawini. Mshauri Msaliboko anaona mlalamikaji arudishwe kazini. Hapa tutie maanani zile barua alizoandika kwa Mwenyekiti baada ya kumwona. Tukumbuke muda mrefu ulipopita aliamua kwenda kulalamika Makao Makuu ya JUWATA. Makao Makuu ya JUWATA walimwagiza aanzie ngazi ya chini kabisa na akafanya hivyo. Haieleweki kwa nini mwishowe Makao Makuu JUWATA waliamua kusema hawangeshughulikia shauri hilo kwa kuwa waliamua kwamba alichelewa kulalamika kwa kuwa alianza kulalamika mara baada ya kuachishwa kazi. Mwisho alilalamika kwa Waziri naye akalipeleka shauri kwa Kamishna wa Kazi. Isanzu aliyekuja kutoa ushahidi kwa ajili ya menejimenti hakuwapo wakati wa matukio haya; alieleza kuwa kutokana na kumbukumbu Kautipe alistaafishwa kwa haki. Upande wa Menejimenti haukuona ulazima wa kuleta ushahidi wa kupinga hoja za Kautipe kama tulivyoziona katika ushahidi wake. Kuna ushahidi katika kumbukumbu kwamba Tawi la JUWATA mahali pa kazi lilimuunga mkono isipokuwa lilifikiri kwa kuwa Kautipe alipokea haki zake, basi shauri lilikwisha. Hakuna ushahidi kwamba Kautipe aliomba kustaafu wala msingi wa kufanya hivyo haukuwapo kwa kuwa umri wake ulikuwa miaka 47 wakati alipostaafishwa. Kulikuwapo wakuu wengi wa Idara siku ya kile kinachodaiwa kuwa ni kikao halali cha tarehe 15/3/83 kilihudhuriwa na wajumbe kumi na mmoja.

Kutokana na barua aliyoandikiwa Kautipe inaelekea (huyu mlalamikaji) hakuitwa kwenye kikao hicho na inaelekea kikao kilimwachisha kazi kwa kusema anastaafishwa kwa maombi yake. Lakini ukweli ni kuwa walimstaafisha kwa kutokana na mwenendo, tabia yake na utendaji wake wa kazi mbaya kwa kipindi ambacho kampuni ilikuwa imewaajiri wahasibu wakuu wapya. Kama sababu ni hizo, Kampuni ingemchukulia hatua za nidhamu kwa kumfungulia mashtaka na kumpa nafasi ajieleze kisha kufuata taratibu zilizowekwa na SCOPO.

Kwa kuwa utaratibu uliofuatwa ni batili uamuzi huo ni batili. Naambatanisha uamuzi na kuamuru mlalamikaji arudishwe kazini bila kupoteza haki zake.

Uamuzi huu umetolewa nami na kushuhudiwa na mkono wangu hapa Dar es Salaam leo tarehe Mosi mwezi wa Novemba, 1989.

J. C. RWEGASIRA, Mb.
Waziri wa Kazi, Utamaduni na Ustawi wa Jamii

CORAM: D. S. Meela—Mwenyekiti
Nd. Msaliboko—Mshauri (JUWATA)
Nd. Nyange—Mshauri (ATE)

TUZO

Tuzo hii imetolewa nami na kushuhudiwa na Muhuri wa Mahakama ya Kazi leo hapa Dar es Salaam siku ya Alhamisi tarehe 23 Novemba, 1989 na inakuwa na nguvu za sheria mara moja.

D. S. MEELA,
Mweyekiti
Mahakama ya Kazi

Certified true copy of the Original

B. E. NYAMUBI,
Registrar

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 197

MAHAKAMA YA KAZI

MGOGORO WA KIKAZI NA. 10 WA 1987

baina ya

JUMUIYA YA WAFANYAKAZI TANZANIA—(JUWATA) DAR ES SALAAM

na

NEW AFRICA HOTEL—DAR ES SALAAM (MWAJIRI)

UAMUZI

Nilitoa kibali kwa Kamishina wa Kazi apeleke mgogoro huu Mahakama ya Kazi ili ufanyiwe uchunguzi chini ya kifungu cha 9A(1) cha Sheria ya Mahakama ya Kazi Na. 41 ya 1967 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 18 ya 1977 ili baada ya uchunguzi nilete taarifa nami nitoe uamuzi wa mgogoro huu chini ya kifungu cha 9B cha Sheria hiyo ya Mahakama ya Kazi.

Mahakama ya Kazi yameshafanya uchunguzi na kunileta taarifa ambayo uamuzi wake ndio huu hapa chini. Wakati naagiza uchunguzi ufanyike, niliagiza yafuatayo yatiliwe maanani sana wakati wa uchunguzi:

(a) Uhalali na utaratibu uliofuatwa na utawala wa hoteli ya "New Africa" kuwapunguza kazi Ndugu Hassani Ali na wenzake.

(b) Masula yoyote ya kisheria yanayojitokeza katika mgogoro huu.

Katika uchunguzi uliofanyika imeonyesha kuwa wafanyakazi waliostaafishwa kazi walikuwa 28 lakini waliolalamika ni wafanyakazi 15 tu. Hivyo uamuzi huu unawahusu wafanyakazi hao 15 na sio wengine. Orodha yao ni kama ifuatavyo:

(1) Hassani Ali
(2) Nassor A. Ahmed
(3) Apolo Mloka
(4) Amani Mohamed
(5) Bakari Ndumbaro
(6) Christina Ombay
(7) Stella Kamalamo
(8) Ali Mtowela
(9) Aisha Semiti
(10) Ramadhani Heri
(11) Bernard Makunja
(12) Seba Duma
(13) Zaituni Maftah
(14) Eliza Lucas
(15) Renson Urasa

Chanzo cha mgogoro huu ni mwajiri kuwastaafisha jumla ya wafanyakazi wake 28 mwaka 1985 kutokana na agizo la serikali la kupunguza ajira na kuongeza tija. Jambo la kustaafisha wafanyakazi licha ya kuwa liliagizwa na serikali, Sheria ya Usalama Kazini Cap. 574 kifungu cha 6(1) (g) kilisharuhusu kustaafisha wafanyakazi mwajiri anapoona kuna umuhimu wa kufanya hivyo, mradi tu mwajiri awasiliane na tawi la JUWATA mahali pa kazi kabla ya utekelezaji wa azma hiyo. Kifungu hicho cha Sheria kinasema:—

"S. 6(1) The functions of a commitee is, and in relation to, the business for which it is established are:—

(g) to consult with the employer concerning any impending redundancies and the application of any joint agreement on the redundancies."

JUWATA kwa niaba ya walalamikaji walidai mahakamani ingawaje kuna uhalali katika kustaafisha wafanyakazi, utaratibu wake (chini ya kifungu nilichonukuu hapo juu) haukufuatwa, yaani kuwasiliana na tawi la JUWATA mahali

pa kazi kabla ya utekelezaji wa agizo la kupunguza ajira. Pia walalamikaji walidai katika madai yao kuwa baada ya wao kustaafishwa menejiment iliajiri wafanyakazi wengine katika nafasi zao, kinyume na taratibu kuhusu sheria ya kustaafisha wafanyakazi. Kutokana na hayo, JUWATA iliomba wafanyakazi 15 niliowataja hapo juu warudishwe kazini bila kupoteza haki zao.

Baada ya madai hayo, menejimenti ilikubali kuwa ni kweli waliwastaafisha wafanyakazi 28 kutokana na agizo la serikali na kuwa waliwalipa stahili zao kwa kiasi cha jumla ya Sh. 585,488.70. Kadhalika menejimenti walikubali kuwa hawakuhusisha tawi la JUWATA mahali pa kazi katika utekelezaji wa agizo hilo kwa mara ya kwanza lakini baada ya malalamiko ya wafanyakazi walirudia tena zoezi hilo na kuwahusisha JUWATA mahali pa kazi.

Mwenyekiti wa JUWATA tawi la "New Africa Hotel" aliiambia mahakama kuwa yeye alikuwa na wadhifa huo tangu 1982 hadi sasa na kuwa japokuwa hawakuhusishwa katika zoezi hili mara ya kwanza hapo tarehe 20/3/85 wafanyakazi 28 walipostaafishwa kulifanyika kikao cha pamoja (JUWATA na Menejimenti) hapo tarehe 11/11/85 na kufanya mkataba baada ya menejimenti kukubali kuwa walikosea utaratibu, na kukubali kuwa waliostaafishwa warudishwe kazini ila kitendo hicho hakikuzuia zoezi lisirudiwe kihalali. Hivyo tarehe 11/11/85 zoezi lilirudiwa na kati ya wafanyakazi wote waliokuwa wamestaafishwa, wanne (4) wao walirudishwa kazini. Wengine 28 waliidhinishwa kustaafishwa. Hata hivyo, ingawaje mkataba ulisema wote warudishwe kwanza kazini ndipo zoezi lifanyike, hakuna aliyerudishwa au kulipwa haki zake kwa kipindi hicho ambacho zoezi lilikuwa batili. Menejimenti walidai kuwa ingekuwa inaongeza gharama badala ya kupunguza, hasa ukitilia maanani kuwa wafanyakazi walikuwa wameshalipwa jumla ya Sh. 588,488.70 na wengi wao wakiwa wameshaondoka hapa mjini na kurudi makwao.

Ili kuweza kuelewa vizuri maamuzi ya kikao cha pamoja cha tarehe 11/11/85, napenda kunukuu sehemu muhimu ya mkataba huo uliotolewa kama kielelezo D_1 mahakamani kama ifuatavyo:—

> "Sisi tujulikanao kama jumuiya ya Wafanyakazi wa Tanzania (JUWATA nasi tujulikanao kama "New Africa Hotel" (WAAJIRI) tunakubaliana kwa pamoja kuwa wafanyakazi walikuwa wameachishwa kazi na NAH kwa zoezi la kubana matumizi na kuongeza tija sasa wanarejeshwa kazini wote na kulipwa haki zao za nyuma.
>
> Kurudishwa kwao kazini hakutazuia zoezi hili kufanyika katika misingi ya kushirikishwa matawi ya CCM na JUWATA mahali pa kazi na kwa misingi iliyomo katika utaratibu wa Sheria na Kanuni za SCOPO."

Makubaliano hayo yalitiwa sahihi na DW_1 Ndugu Mwakasagule kwa niaba ya tawi la JUWATA na Ndugu E.A. Kazoka kutoka JUWATA Makao Makuu kwa upande wa Wafanyakazi na Meneja utawala alitia sahihi kwa niaba ya "New Africa Hotel" mnamo tarehe 11/11/85.

Ushahidi uliotolewa mahakamani bila kupingwa ni kuwa menejimenti walitekeleza aya ya pili ya mkataba wa kurudia tena kwa upya zoezi la kupunguza ajira na wakaacha aya ya kwanza ya kuwarudisha kazi wafanyakazi na kuwalipa haki zao za kuanzia 21/3/85 hadi 16/11/1985. hapo ndipo menejimenti ilipoonyesha dhamira yao ya kutotekeleza Sheria ya Usalama Kazini au hata kutekeleza masharti ya mkataba wao na JUWATA. Walitoa sababu za kutokuwa na fedha na walalamikaji wakashikilia haki zao.

Wakati walipotoa hoja zao za mwisho kwa njia ya maandishi menejimenti walidai kuwa kati ya hao walalamikaji 15, ni watano (5) tu ambao hawajaajiriwa na wengine, kuanzia mlalamikaji Na. 6 hadi Na. 15 yaani Christina Ombay hadi Renson Urasa (katika orodha hapo juu) wameajiriwa mahali pengine. Hawakueleza mahali kila mmoja wao alipoajiriwa wala tarehe ya kuajiriwa. Siyo hilo tu, bali tena hawakueleza hivyo wakati DW_1 alipotoa ushahidi mahakamani ili aweze kuhojiwa na JUWATA kwa niaba ya walalamikaji. Hii ina maana kuwa hao walalamikaji wanaweza kufaidika mara mbili au wasifaidike na uamuzi huu kama uchunguzi zaidi haukufanyika.

Katika madai ya JUWATA hapo awali, walidai kuwa kuliajiliwa wafanyakazi wengine baada ya hao kustaafishwa, lakini nao hawakuutoa ushahidi wowote kuhusu suala hilo mahakamani. Hivyo madai hayo yanafutwa kwani hayana ushahidi wowote ule.

Katika zoezi lote la kustaafisha wafanyakazi 28 na hatimaye 15 kulalamika, ushahidi umeonyesha kuwa zoezi lilikuwa halali lakini utaratibu haukufuatwa kwa kutowasiliana na JUWATA mahali pa kazi kwa mara ya kwanza. Kitendo hicho kinabatilisha zoezi hilo kuanzia tarehe 21/3/85 hadi tarehe 16/11/1985 wakati zoezi liliporudiwa na kuhusisha tawi la JUWATA mahali pa kazi. Baada ya tarehe 16/11/85 zoezi lilikuwa halali na utaratibu ulifuatwa. Hivyo ina maana kuwa wafanyakazi walitakiwa warudishwe kazini kwa kipindi hicho cha kuanzia 21/3/1985 hadi 16/11/85. Pili, ukitilia maanani hoja za mwisho za mwajiri, wafanyakazi kumi (10) itakuwa wathibitishe tarehe walizoajiriwa na mwajiri mwingine ili wastahili hayo malipo. Hii ina maana kila mmoja wao, kuanzia Na. 6 hadi 15 katika orodha niliyotaja hapo juu, atalipwa tu kwa zile siku ambazo alikuwa hajaajiriwa kati ya tarehe 21/3/85 na 16/11/85. Menejimenti ya New Africa Hotel watapata uthibitisho kutoka kwa waajiri wapya tarehe wayoajiriwa mara baada ya kustaafishwa nao. Hii ni kuepuka mfanyakazi asije akapata mishahara mara mbili kwa kipindi hicho hicho.

Hivyo basi natoa uamuzi kuwa kuwastaafisha wafanyakazi 15 waliolalamika kati ya tarehe 21/3/85 hadi 16/11/85 kulikuwa kwa makosa na ninabatilisha uamuzi huo. Wafanyakazi Hassan Ali, Nassor A. Ahmedi, Apolo Mloka, Amani Mohamed na Bakari Ndumbaro walipwe mishahara yao yote ya kipindi cha kuanzia tarehe 21/3/85 hadi 16/11/85 bila kurudishwa kazini na wafanyakazi wengine 10 waliobaki, walipwe mishahara yao baada ya kutoa barua za waajiri wao wa sasa kuonyesha ni tarehe gani waliajiriwa ili pasiwe na yeyote atakayelipwa mishahara miwili kwa kipindi hicho; na ninafunga mgogoro huu.

Uamuzi huu umetolewa nami na kushuhudiwa na mkono wangu hapa Dar es Salaam leo tarehe 29 mwezi wa Juni, 1989.

Sgn. C. T. KISANJI, MB.
Waziri wa Kazi, Utamaduni na Ustawi wa Jamii

Certified true Copy of the original.

B. E. NYAMUBI,
Registrar

CORAM: A. R. Manento—Naibu Mwenyekiti
Nd. Mwenura—Mshauri (JUWATA)
Nd. C. Y. Isinika—Mshauri (ATE)

TUZO

Tuzo hii imetolewa nami na kushuhudiwa na Muhuri wa Mahakama ya Kazi leo hapa Dar es Salaam siku ya Jumanne tarehe 25/7/89 na inakuwa na nguvu za sheria mara moja.

Sgn. A. R. MANENTO,
Naibu Mwenyekiti Mahakama ya Kazi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 198

UTHIBITISHO NA USIMAMIAJI WA MIRATHI

(Katika Mahakama ya Hakimu Mkazi, Dar es Salaam)

SHAURI LA MIRATHI NA. 26 LA MWAKA 1990

Maombi ya barua za Usimamiaji wa Mirathi ya Abubakar Minchum, Marehemu

na

Hassan Abubakar, Mwombaji

TAARIFA YA KAWAIDA

(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika Mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa Wasia/Barua za Usimamiaji wa Mirathi kwa muombaji aliyetajwa hapo juu/ kwa waombaji waliotajwa hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 16 mwezi wa Juni, mwaka 1990.

Wasia wa marehemu huyo aliyetajwa umewekwa kwa amana na uwazi kwa upekuzi Mahakamani.

Imewasilishwa Dar es Salaam leo tarehe 16 mwezi Machi, mwaka 1990.

.....

Hakimu Mkazi Mkuu

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 199

UTHIBITISHO NA USIMAMIAJI WA MIRATHI

(Katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkuu Kisutu, Dar es Salaam)

SHAURI LA MIRATHI NA. 25 LA MWAKA 1990

Maombi ya barua za Usimamiaji wa Mirathi ya Ratilal Narandas Simzia, Marehemu

na

Kaushik Ratillal Narandas Simzia and Kishore Ratilal Narandas Simzia, Waombaji

TAARIFA YA KAWAIDA

(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanaombwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada hili kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua za Usimamizi wa mirathi kwa waombaji waliotajwa hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 23 mwezi wa Juni mwaka 1990.

Imewasilishwa Dar es Salaam leo tarehe 23 mwezi Machi, 1990.

I. H. M. MAGESA,
Hakimu Mkuu Mkazi
Kisutu, Dar es Salaam

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 200

UTHIBITISHO NA USIMAMIAJI WA MIRATHI

(Katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Dar es Salaam)

SHAURI LA MIRATHI NA. 63 LA MWAKA 1989

Maombi ya barua za Usimamiaji wa Mirathi ya Frank John Mbwambo, Marehemu

na

Edson John Mbwambo, mwombaji

TAARIFA YA KAWAIDA

(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu.

Wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa Wasia/Barua za usimamiaji wa Mirathi kwa muombaji aliyetajwa hapo juu/kwa waombaji waliotajwa hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya y[illegible] yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 6 mwezi wa [illegible] mwaka 1990.

Imewasilishwa Dar es Salaam leo tarehe 6 mwezi Februari, 1990.

.....

Naibu Msajili Mwandamizi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 201

UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI

(Katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Dar es Salaam)

SHAURI LA MIRATHI NA. 12 LA MWAKA 1990

Maombi ya barua za Usimamizi wa Mirathi ya Omari Selemani, Marehemu

na

Hassan Omari, Mwombaji

TAARIFA YA KAWAIDA

(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa Wasia/Barua za usimamiaji wa mirathi kwa mwombaji aliyetajwa hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 20 mwezi Mei, mwaka 1990.

Wasia wa marehemu huyo aliyetajwa umewekwa kwa amana na uwazi kwa upekuzi Mahakamani.

Imewasilishwa Dar es Salaam leo tarehe 15 mwezi Februari 1990.

.....

Naibu Msajili

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 202

UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI

(Katika Mahakama ya Hakimu Mkuu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam)

SHAURI LA MIRATHI NA. 30 LA MWAKA 1990

Maombi ya barua za Usimamizi wa Mirathi ya Francis Augustine Mowo, Marehemu

na

Lydia Francis Mowo, Mwombaji

TAARIFA YA KAWAIDA

(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa miradhi kwa mwombaji aliyetajwa hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 28 mwezi Mei, 1990.

Imetolewa Dar es Salaam leo tarehe 28 mwezi Machi, 1990.

.....

Hakimu Mkuu Mkazi, Dar es Salaam

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 203

UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI

(Katika Mahakama ya Hakimu Mkuu Mkazi, Kisutu Dar es Salaam)

SHAURI LA MIRATHI NA. 23 LA MWAKA 1990

Maombi ya barua za Usimamizi wa Mirathi ya Jonathan Petro Mkwavi, Marehemu

na

Michael Jonathan Mkwavi, Mwombaji

TAARIFA YA KAWAIDA

(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa usimamizi wa mirathi kwa mwombaji aliyetajwa hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 13 mwezi Juni, 1990.

Imetolewa Dar es Salaam leo tarehe 13 mwezi Machi, 1990.

.....

Hakimu Mkuu Mkazi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 204

UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI

(Katika Mahakama ya Hakimu Mkuu Mkazi, Dar es Salaam)

SHAURI LA MIRATHI NA. 131 LA MWAKA 1989

Maombi ya barua za Usimamizi wa Mirathi ya Hilali Mahundi, Marehemu

na

Esteria Kipanga, Mwombaji

TAARIFA YA KAWAIDA

(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji aliyetajwa hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 15 Machi, 1989.

Imewasilishwa leo tarehe 18 mwezi Desemba, 1989.

.....

Hakimu Mkuu Mkazi, Dsm

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 205

UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI

(Katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Dar es Salaam)

SHAURI LA MIRATHI NA. 67 LA MWAKA 1989

Maombi ya barua za Usimamizi wa Mirathi ya Ibrahim Abdallah, Marehemu

na

Shaban Yusufu, Mwombaji

TAARIFA YA KAWAIDA

(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa Wasia/Barua za usimamiaji wa mirathi kwa mwombaji aliyetajwa hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 6 mwezi wa Aprili, mwaka 1990.

Wasia wa marehemu huyo aliyetajwa umewekwa kwa amana na uwazi kwa upekuzi Mahakamani.

Imewasilishwa Dar es Salaam leo tarehe 19 mwezi Desemba, 1989.

.....

Naibu Msajili

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 206

UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI

(Katika Mahakama ya Hakimu Mkuu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam)

SHAURI LA MIRATHI NA. 28 LA MWAKA 1990

Maombi ya barua za Usimamizi wa Mirathi ya Saidi Bakari Mwenda, Marehemu

na

Athumani Selemani Sekuru, Mwombaji

TAARIFA YA KAWAIDA

(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji aliyetajwa hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 24 mwezi Juni, 1990.

Wasia wa marehemu huyo aliyetajwa umewekwa kwa amana na uwazi kwa upekuzi Mahakamani.

Imewasilishwa Dar es Salaam leo tarehe 24 mwezi Machi, 1990.

I. H. M. MAGESA,
Hakimu Mkuu Mkazi, Dar es Salaam

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 207

DEED POLL

(The Registration of Documents Cap. 117)

By this Deed I, KIVANGWA MAULIDI ATHUMANI KIDESU of Post Office Box Number 912 Dodoma, do hereby absolutely renounce and abandon the use of my former name MAULIDI ATHUMANI and in lieu there of do assume and adopt the name of KIVANGWA MAULIDI ATHUMANI KIDESU.

And in pursuance of such change of name as aforesaid I HEREBY DECLARE THAT I shall at all times hereafter in all records, deeds and instruments, in writing and in all actions and proceedings and in all dealings and transections and upon all occassions whatever use and sign the said name of KIVANGWA MAULIDI ATHUMANI KIDESU as my name in lieu of the said MAULIDI ATHUMANI renounced as aforesaid.

And I HEREBY authorise and request all persons to designate and address me in the name of KIVANGWA MAULIDI ATHUMANI KIDESU on the day and in the manner hereinafter appearing.

SIGNED AND DELIVERED by the said KIVANGWA MAULIDI ATHUMANI KIDESU who is known to me personally in my presence this 25th day of February, 1990.

NAME: RIDHARD RWEYONGEZA
SIGNATURE:.....
QUALIFICATION: ADVOCATE.
CCT CHURCH HOUSE,
P.O. BOX 1013,
DODOMA.

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 208

MALI ISIYOKUWA NA MWENYEWE

(In the District Court of Geita District at Geita)

(The Police Force Ordinance, Cap. 322, Section 44)

WHEREAS the property described in the Schedule hereto has been handed to or found by the Police and no claim to the ownership thereof has been received: notice is hereby given that unless any person who may have a claim thereto appears and establishes his claim within six months from this date the said property may be sold and the proceeds thereof dealt with according to law.

Dated this 14th day of March, 1990.

A. L. E. KYEBYALA,
Principal District Magistrate

SCHEDULE

Item No.	*Description of Property*
BUT/RB/93/87	Baiskeli moja aina ya Steel No. GL 00883 Nyekundu
BUT/RB/11/88	Fremu moja ya Baiskeli aina ya Flying Pegeon pamoja na Ringi mbili.
BUT/RB/227/89	Ng'ombe mmoja jike.

Kuajiriwa na Kukabidhiwa Madaraka—(inaendelea kutoka ukurasa wa 87)

Kuwa Wapiga Taipu Daraja la II:—

EDINA LIFA, kuanzia tarehe 16 Juni, 1989.
NUWIYA NASSORO, kuanzia tarehe 16 Juni, 1989.
JANE MASWE, kuanzia tarehe 16 Juni, 1989.
OSWINA M. MAILLEH, kuanzia tarehe 16 Juni, 1989.

Wizara ya Mawasiliano na Ujenzi—Idara Kuu ya Hali ya Hewa:

Kuwa Meteorologist Grade III:—

F. TILLYA, kuanzia tarehe 1 Machi, 1990.
I. NASSIB, kuanzia tarehe 1 Machi, 1990.
H. M. MCHOMBA, kuanzia tarehe 1 Machi, 1990.
J. H. ALIBA, kuanzia tarehe 1 Machi, 1990.
M. A. MGENDI, kuanzia tarehe 1 Machi, 1990.

Wizara ya Viwanda na Biashara:

Kuwa Wasajili Wasaidizi III:—

E. E. MAHINGILE, kuanzia tarehe 1 Machi, 1990.
K. KISHEBUKA, kuanzia tarehe 1 Machi, 1990.
B. GOGADI, kuanzia tarehe 1 Machi, 1990.

Kuwa Maafisa Biashara II:—

C. F. OWENYA, kuanzia tarehe 1 Oktoba, 1989.
D. F. MWASEBA, kuanzia tarehe 1 Oktoba, 1989.

SAHIHISHO

Supplement Na. 12 ya tarehe 23 Machi, 1990. Government Notice Na. 73 imeandikwa mara mbili, kwa hiyo kati ya hizo mbili Government Notice ya mwisho *Isomeke* Na. 74.

Limepigwa chapa na Mpigachapa wa Serikali, Dar es Salaam—Tanzania